# Nipashe

Jumatatu Novemba 9, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580394

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital ni… nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


**NECTA** yaonya uhujumu mitihani

UKURASA 3



**RAIS** Mwinyi amteua Makamu wa Pili wa Rais

UKURASA 8



**Deschamps atoa neno kumwacha Upamecano**

UKURASA 20

# Saruji haishikiki

• **Yaadimika** kila mahali nchini, mfuko wafikia 35,000/-, wananchi waiangukia serikali... *Endelea ukurasa 4*




Baadhi ya malori yakiwa yameegeshwa kusubiri kupakia saruji na mengine yakisubiri kutoka katika eneo la Tegeta Wazo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mvua kubwa kunyesha siku tano

UKURASA 2

## NEC yatangaza viti maalum, CHADEMA yaambulia 19

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

SALAMU ZA PONGEZI



Gazeti Nipashe linampongeza Rais Dkt John Magufuli na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha Miaka 5. 2020 - 2025

Kwa salamu za pongezi
Wasiliana nasi kwa Simu: 0686 101335
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



SALAMU ZA PONGEZI

HABARI KITAIFA

## Mvua kubwa kunyesha siku 5

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA), jana, imetoa utabiri ukionyesha kuwapo kwa mvua kubwa kwa siku tano kuanzia jana Jumapili katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Tanga na Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mamlaka hiyo kupitia kitengo cha habari, mvua inatarajiwa kunyesha kwenye baadhi ya maeneo ya mikoa hiyo kwa siku tano mpaka Jumatano.

"Mvua hiyo tunatarajia itafikia mwisho Jumatano, mamlaka inaendelea kufuatilia kwa karibu mabadiliko yoyote yanayoweza kutokea," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema wanatarajia athari mbalimbali zitatokea kwa wananchi na maeneo yao.

"Kwa kiasi kikubwa mvua hiyo itasababisha kutuama kwa maji kwa baadhi ya maeneo ya makazi ya watu, lakini inaweza ikaleta uharibifu wa miundombinu," ilisema taarifa hiyo.

Mamlaka hiyo imewataka wananchi wa maeneo hayo, kuchukua tahadhari kuepukana na athari hizo huku pia mamlaka husika zikitakiwa kuchukua tahadhari ya uharibifu wa miundombinu kwa kuamua kusafisha mitaro, ili kupitisha maji kwa urahisi.

Mchambuzi wa hali ya hewa wa mamlaka hiyo, Joyce Makwata, alisema mvua wanatarajia itafika kikomo Jumatano.

"Mvua hiyo inatokana na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyoonekana, TMA itaendelea kutoa taarifa kwa wananchi kila panapotokea mabadiliko," alisema Joyce.

# NEC yaanika viti maalum, CHADEMA yaambulia 19

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeweka wazi idadi ya wabunge wa viti maalum iliyoonyesha Chama Cha Mapinduzi(CCM) kimepata nafasi 94, huku Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA) kikipata nafasi 19.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Charles Mahera, alisema majina yalishatangazwa na yamewasilishwa bungeni.

"Mkiyahitaji mtayapata huko huko (bungeni), CCM 94 na CHADEMA 19, vyama vingine havina sifa ya kupata viti maalum," alisema.

Alipoulizwa kuhusu orodha ya majina ya wabunge hao, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, alisema alishatangaza utaratibu wa kujisajili kwa wabunge wote wakiwamo wa viti maalum, ambapo usajili huo ulianza juzi na utamalizika leo.

"Usajili unaendelea kwa wabunge wote na wanatakiwa kwenda na cheti ya kuteuliwa au kuchaguliwa wanavyopewa na NEC, na orodha yao nitaipata vizuri wakikamilisha kujisajili," alisema.

Vyama hivyo vilivyopata wabunge wa viti maalum vimepata asilimia tano ya kura halali za wabunge.

Katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, Rais John Magufuli aliibuka kwa ushindi wa kura milioni 12.5 huku mpinzani wake wa karibu, Tundu Lissu wa CHADEMA, akipata kura milioni 1.9.

Aidha, baada ya matokeo hayo yaliyowaangusha vigogo wengi wa CHADEMA , akiwamo Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe, kwa pamoja na Chama cha ACT-Wazalendo, walitangaza kutotambua matokeo hayo na hawatashirikiana na serikali zaidi atajikita katika kudai katiba mpya kupitia maandamano ya amani, ambayo hata hivyo hayakufanyika baada ya viongozi wakuu kukamatwa na polisi.




Mbunge mteule Jimbo la Hai (CCM), Shaashisha Mafuwe (kulia), akijisajili ofisi za Bunge jijini Dodoma, alipofika kwa ajili ya usajili wa wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kushoto ni ofisa wa mbunge, Felister Mgonja.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wabunge wateule wataja vipaumbele vyao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wateule wa Bunge la 12, wamefunguka namna watakavyowakilisha wananchi wao bungeni, huku wakitaja vipaumbele wanakavyoanza navyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana kwenye viwanja vya Bunge baada ya kujisajili, walishukuru wananchi wa majimbo yao kwa kuwachagua na kuahidi hawatawaangusha.

Mbunge Mteule wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alisema kazi imeanza baada ya uchaguzi kumalizika na wananchi wa jimbo hilo wamemtuma mambo mengi ya kuwasemea bungeni.

"Zipo kero za kutosha kwenye suala la maji, barabara ni imani yangu tunaenda kuzitatua zote kwa kuwa yapo kwenye Ilani ya uchaguzi, kazi yangu ni kuunganisha serikali na wananchi tuende kwa kasi, yale niliyokuwa nazungumza naenda kuyafanya kwa vitendo," alisema.

Alisema kipaumbele cha jimbo hilo ni kilimo na viwanda hivyo dhamira yake ni kuimarisha uchumi wa mtu mmoja kupitia kilimo na viwanda.

"Kama mnavyojua Jimbo la Hai tumekuwa kwenye upinzani takribani miaka 20, kwa hiyo wana kiu kubwa ya kuona utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, nitasimamia utekelezaji kwa asilimia 100, lakini kuisimamia serikali kutekeleza ahadi zilizotolewa na viongozi wakuu kwenye kampeni, kwa kasi kubwa tunaenda kuonyesha tofauti ya kuchagua CCM," alisema.

Alisema kwa sasa anapita kata zote kuwauliza wananchi mambo ambayo wanataka wawakilishiwe bungeni.

"Ninachofanya kwa sasa kabla ya kuapishwa nimeanza kuzungumza baadhi ya kata na kuzungumza na wananchi ni mambo gani wanataka niwawakilishie bungeni," alisema.

Mafuwe alimkaribisha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Freeman Mbowe, kumpa ushauri na maoni yake kwa kuzingatia Ilani ya CCM.

"Yule ni mwananchi katika jimbo langu na anazoheshima kama kiongozi mstaafu wa Jimbo la Hai," alisema. Mbunge Mteule wa Shinyanga Mjini (CCM), Patrobas Katambi, alisema kwa sasa ana deni kubwa na ana dhamira ya kuongeza kasi kubadili uchumi na mzunguko wa fedha kwenye jimbo hilo ndani ya miaka mitano ijayo. Alisema kwa sasa anaangalia namna ya kutengeneza maeneo kwa ajili ya biashara ya ufungaji, ujenzi wa shule, chuo kikuu ili kuongeza mzunguko wa fedha.

Alisema atahakikisha anashughulikia suala la ajira kwa vijana wanaomaliza na kushindwa kuajiriwa na kuhakikisha mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

**MBUNGE UPINZANI**

Mbunge Mteule wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema kazi aliyoomba kuwatumikia wananchi wake ndio imeanza rasmi.

"Nipo hapa kwa kupitia CHADEMA, sijahama na ni mbunge halali, hayo mengine yanayoendelea nitasubiri utaratibu nitakaopewa kwa kuwa CHADEMA ni taasisi, nawashukuru wanaNkasi kwa heshima niwaambie wana Nkasi Kaskazini kazi ndio imeanza," alisema.

Kadhalika, Mbunge Mteule wa Nyasa (CCM), Stella Manyanya, alisema suala la maji ni kero kubwa na watu wanatumia muda mwingi kuyafuata.

Aliahidi kuhakikisha anashughulikia tatizo hilo ili kuchochea kasi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa viwanda vidogo.

Manyanya aliwashukuru wananchi wa jimbo hilo na kueleza kuwa uchaguzi umeisha na kwa sasa ni kazi tu na kipaumbele cha kwanza ni kushughulikia tatizo hilo la maji.

Mbunge Mteule wa Kilindi, Omary Kigua, alisema ndani ya miaka mitano ijayo amejipanga kuwatumikia kwa nguvu mpya ili kuhakikisha changamoto zilizobaki ikiwano suala la miundombinu ya barabara kwenye baadhi ya vijiji zinatengenezwa ili zipitike kwa urahisi. Mbunge Mteule wa Same Mashariki, Anne Kilango Malecela, alisema amefurahi kurejea bungeni kwa kipindi kingine kutokana na miaka mitano iliyopita kupoteza jimbo hilo.

Alisema aliumizwa kupoteza ubunge miaka mitano iliyopita licha ya kwamba rais alimteua, lakini anashukuru Mungu kwa sasa amerejea kuwatumikia wananchi wa jimbo hilo.

Katika usajili huo wabunge hao wanapewa nyaraka mbalimbali ikiwamo Katiba, Kanuni za Bunge na Kishikwambi (tablet).

## HABARI KITAIFA

# Jela miaka 20 kujaribu kumlawiti mwanafunzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kata ya Mnazi-Mmoja, Manispaa ya Lindi, mkoani hapa, Mohamedi Abdallah (50), amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 20 jela, baada ya kukutwa na hatia ya kujaribu kulawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 14, jina limehifadhiwa.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Lindi, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa pasipo shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, wakiwamo wanafunzi wenzake waliojitokeza kumwokoa.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa iwapo ana lolote litakaloishawishi Mahakama isimpe adhabu kali kutokana na kuomba aonewe huruma akidai ni mkosaji wa mara ya kwanza, na pia anayo familia inayomtegemea akiwamo mke na watoto.

"Mheshimiwa nakiri kutaka kufanya tendo hilo, baada ya ibilisi kunipitia, hivyo basi naiomba Mahakama yako tukufu inionee huru kwani nina familia inanitegemea...ukinipa adhabu kali itashindwa kupata malezi yangu," alidai mshtakiwa.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Emmanuel John, aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya aina hiyo, kwa madai mshtakiwa ni mzoefu, na amekuwa na tabia hiyo kwa muda mrefu.

Hakimu Batraine akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 79/2020, kupitia vifungu 154 na 155 kifungu kidogo cha kwanza (a) kanuni ya adhabu sura ya 16 rejeo la mwaka 2019, alimhukumu mshtakiwa Abdallah, ambaye ni fundi viatu kutumikia kifungo cha miaka 20 gerezani.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na John kuwa Agosti 02 mwaka huu, majira ya mchana, mshtakiwa akiwa katika mizunguko yake alikutana na mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi anayesoma darasa la tatu Shule ya Msingi Mingoyo, alimlaghai kwa kumpa Sh. 500.

John alidai mlalamikaji alipokataa kupokea fedha hizo, mshtakiwa alitumia mabavu kwa kumshika mkono, huku akimtishia kwa kisu iwapo atakataa amri yake na kumpeleka kwenye kichochoro kilichopo eneo la Shule ya Sekondari Mingoyo, huku likishuhudiwa na mwanafunzi mmoja, ambaye alifuatilia tukio hilo.

Alidai baada ya kubaini dhamira ya mshtakiwa, mwanafunzi huyo na kuwapa taarifa wenzake, ambao walikwenda eneo la tukio na kumkuta mshtakiwa amevua nguo zake tayari kutekeleza alichokusudia.

John alidai kuwa wanafunzi hao walimkamata mshtakiwa na kumpeleka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Muungano, Juma Fumaao.

# NECTA yaonya wahujumu mitihani ya upimaji

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani Tanzania (NECTA), limeonya watu au vikundi vya watu vilivyojipanga kuhujumu mitihani ya upimaji darasa la nne, kidato cha pili na mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne ambayo itafanyika kwa siku tofauti kuanzia leo, kuwa litawachukulia hatua za kisheria.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mitihani hiyo ambayo kwa leo upimaji wa kitaifa wa Kidato cha Pili utafanyika hadi Novemba 20 katika jumla ya shule 4,948 Tanzania Bara.

Alisema Baraza linawaasa wasimamizi, wamiliki wa shule, walimu na wazazi au walezi kutojihusisha au kushiriki kwa namna yoyote na vitendo vya udanganyifu wa mtihani huo.

Dk. Msonde alisema mtihani wa kidato cha nne na maarifa utafanyika kuanzia Novemba 23 hadi Desemba 11, mwaka huu katika jumla ya shule za sekondari na vituo vya mtihani 6,727 Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

"Upimaji wa darasa la nne utafanyika kwa siku mbili kuanzia Novemba 25 katika jumla ya shule za msingi 17,812 Tanzania Bara," alisema.

Alisema jumla ya watahiniwa 1,825,679 wamejasiliwa kufanya upimaji wa kitaifa wa darasa la nne na kati yao wavulana ni 909,068 sawa na asilimia 49.8 na wasichana ni 916,611, asilimia 50.2.

"Wenye mahitaji maalum ni 4,329 ambapo kati yao, wenye uoni hafifu ni 780, wasioona ni 103, wenye ulemavu wa kusikia ni 1,025 na wenye ulemavu wa viungo vya mwili ni 2,421," alisema.

Alisema mwaka jana idadi ya watahiniwa waliosajiliwa ilikuwa 1,783,638 na kufanya ongezeko la jumla ya watahiniwa 42,041 sawa na asilimia 2.30, mwaka huu.

Kwa upande wa kidato cha pili, Dk. Msonde alisema jumla ya watahiniwa 646,148 wamesajiliwa kufanya na kati yao wavulana ni 301,831 sawa na asilimia 46.71 na wasichana 344,317 sawa na asilimia 53.29.

Alisema wenye mahitaji maalum ni 731, kati yao wenye uoni hafifu 406, wasioona 55, wenye ulemavu wa kusikia watatu na wenye ulemavu wa viungo vya mwili 267.

Alisema mwaka jana idadi iliyofanya mtihani huo wa upimaji ilikuwa 609,502 ikilinganishwa na ya mwaka huu, kuna ongezeko la watahiniwa 36,646 sawa na asilimia 5.7.

Dk. Msonde alisema watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani wa kidato cha nne ni 490,103 kati yao watahiniwa wa shule ni 448,164 na wa kujitegemea ni 41,939.

Alisema kati ya watahiniwa wa shule waliosajiliwa, wavulana ni 213,553 sawa na asilimia 47.7 na wasichana 234,611 sawa na asilimia 52.3, wenye mahitaji maalum ni 893.

Alisema kati ya wenye mahitaji maalum, wenye uoni hafifu ni 425, wasioona ni 60, wenye ulemavu wa kusikia 186 na wenye ulemavu wa viungo vya mwili, 222.

Alisema kwa mwaka jana waliofanya mtihani huo walikuwa 485,866 na kufanya ongezeko la watahiniwa 13,663 sawa na asilimia 2.7, mwaka huu.

Kwa watahiniwa wa kujitegemea ambao jumla yao ni 41,939, alisema wavulana ni 18,118 sawa na asilimia 43.2 na wasichana 23,821, asilimia 56.79.

Alisema wenye mahitaji maalum wapo 11, kati yao walio na uoni hafifu ni saba na wasioona ni wanne na kwamba mwaka jana idadi ya watahiniwa waliosajiliwa ilikuwa ni 52,814.

Kuhusu mtihani wa maarifa alisema jumla ya watakaoufanya ni 9,426, wanaume 4,147 sawa na asilimia 44 na wanawake 5,279 sawa na asilimia 56.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA MKOA KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA 127/2020**

**ADOLPH BANYENZA.........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ARISTIDES MUGOA.........................WAJIBU MAOMBI**
**RICHARD MEYEMELE**
**BONIPHACE PAUL**

**KWA:ARISTIDES MUGOA**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa Maombi Na 127/2020 yamepangwa kutajwa tarehe 13.11.2020 Mbele ya Mwenyekiti wa Baraza J.K. Banturaki saa 2:30 asubuhi,mahali-Muleba (Mamlaka ya Mji Mdogo.
Hivyo,unaamuriwa kuhudhuria mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 26.10.2020

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MULEBA



**KATIKIA MAHAKAMA YA MWANZO ISANGA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA.....01....2020**

**OMBI LA JISENGE NDEKAGI kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu MUSA GUDO NDEKAGI**

**Kwa Yeyote anayehusuika**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 02/11/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hio.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

MAHAKAMA YA MWANZO ISANGA

Tarehe: 02.10.2020

Sahihi ya Hakimu



Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

**DIVIDEND ANNOUNCEMENT**

The Annual General Meeting (AGM) of the bank which was held on **29th August, 2020** approved the payment of **Tshs. 22.5** per share as dividend for Financial Year 2019 as submitted by the Board of Directors. Pursuant to the dividend payment declaration, the Share Register details shall remain as follows:

| | | |
|---|---|---|
| Dividend declaration | : | 9th November, 2020 |
| Trading of Shares cum Dividend | : | 9th November 2020 to 26th November, 2020 |
| Trading of shares Ex Dividend | : | 27th November, 2020 on wards |
| Closure of the Members Register | : | 01st December, 2020 |
| Dividend Payment on or by | : | 14th December, 2020 |

Dividend will be paid directly to the Shareholder's bank account for those who have instructed so or through mobile (M-pesa, Tigo pesa, Airtel money, EZY- Pesa)

**BY ORDER OF THE BOARD**

# Bei ya saruji haishikiki

**Na Waandishi Wetu**

BEI ya saruji katika maeneo mbalimbali nchini imepanda, huku ikisababisha gharama za ujenzi kuongezeka na kukwamisha shughuli za maendeleeo ambazo zinategemea bidhaa hiyo.

Katika baadhi ya maeneo kumekuwa na ongezeko la Sh. 3,000 hadi 8,000, mfuko mmoja wa kilo 50 ukiuzwa kwa Sh. 35,000.

Katika baadhi ya viwanda kumeshuhudiwa msururu wa magari yakisubiri bidhaa hiyo, mengi yakitoka nchi za Burundi na Rwanda na kusota kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Wafanyabiashara wa ndani wanaonunua kwa jumla bidhaa hiyo wamejikuta wakisota kwa zaidi ya miezi mitatu bila kupata kiasi walicholipia kiwandani.

Kwa mikoa iliyopakana na Kenya wananchi wananunua saruji ya nje ambayo bei yake ni kati ya Sh. 16,500 hadi 17,000 huku ya nchini ikiuzwa kwa Sh. 24,000.

Tanzania kuna viwanda vya saruji ambavyo uhudumia mikoa na kanda mbalimbali ambavyo ni Twiga Cement, Simba Cement, Nyati Cement, Tanga Cement, Mtwara Cement, Dangote, Mbeya Cement huku Kanda ya Ziwa ikiwa haina kiwanda cha uzalishaji wa bidhaa hiyo. Viwanda vinavyotarajiwa vinavyojengwa maeneo ya Shinyanga na Bunda.



**DAR ES SALAAM**

Maeneo ya Tandika, Temeke, Kibamba, Ukonga na Gongo la Mboto, kwa sasa mfuko mmoja wa saruji unauzwa kati ya Sh. 15,000 hadi 16,000 kutoka Sh. 14,000 hadi 14,500.

Muuzaji wa duka la vifaa vya ujenzi lililopo Mombasa, Ukonga, Jinnihi James, alisema saruji inapokuwa dukani kwake ya Twiga, huuzwa kati ya Sh. 15,000 hadi 16,000 ingawa kwa hivi sasa hana bidhaa hiyo.

"Kwa takribani mwezi mmoja sina saruji, nikiuliza wanaotusambazia mara kwa mara mfano saruji ya Twiga, wanasema uzalishaji umeshuka na mahitaji yapo zaidi," alisema James.

**ARUSHA**

Katika Jiji la Arusha bidhaa hiyo imepanda kutoka Sh. 14,500 hadi 19,000 kwa baadhi ya maduka ya ujenzi kwa kipindi cha miezi mitatu tangu Julai, mwaka huu.

Mfanyabiashara na mmiliki wa duka la ujenzi la Tulivu Hardware, alisema mfuko mmoja wa saruji ya Simba uko juu, tofauti na ya Twiga, Kilimanjaro na Moshi Cement.

**NGORONGORO**

Mfuko mmoja wa saruji ya kampuni ya Simba unauzwa Sh. 25,000 hadi 35,000.

Akizungumza na gazeti hili, Lotha Saigurani, mkazi wa Loliondo, alisema awali walinunua kwa Sh. 10,000 na sasa imepanda zaidi.

Katika Mji Mdogo wa Namanga uliopo mpakani mwa Tanzania na Kenya, saruji inauzwa Sh. 18,000 bei ambayo wameizoea tangu awali.

**TANGA**

Mkoani Tanga ambako kuna kiwanda cha Tanga Cement, bei imepanda kutoka Sh. 12,000 hadi Sh.14,000.

"Ukweli ni kwamba kuna maeneo inauzwa 13,000 na maeneo mengine mpaka 15,000 kwa saruji ya kampuni ya Simba, lakini upo uhaba wa saruji hapa Tanga," alisema Denis Komba, mkazi wa jijini hapa.

**KILIMANJARO**

Mfuko mmoja wa kilo 50 umepanda kutoka Sh. 14,500 hadi Sh. 21,000, huku baadhi ya wafanyabiashara wa jumla wakilalamikia kutopatikana kwa saruji kutoka viwanda vya kutengeneza bidhaa hiyo nchini.

Mmoja wa maofisa masoko wa kiwanda cha saruji cha Moshi (hakutaka kutajwa jina lake) alisema bidhaa hiyo imepanda kutokana na uhitaji kuwa mkubwa sokoni, lakini bado wanawauzia mawakala wao mfuko mmoja kwa Sh. 12,500 na kuwaelekeza wasiuze zaidi ya Sh. 14,000.

**MANYARA**

Mji wa Babati bidhaa hiyo haikamatiki licha ya kuwa adimu, imepanda kutoka 15,000 hadi 20,000.

Mfanyabiashara wa saruji na mkazi wa Babati, Nelson Mosha, alisema hadi sasa hawajui kinachosababisha bidhaa hiyo kupanda bei na kushuka na kuiomba serikali kuingilia kati.

Msimamizi wa Timber & Yard, Emmanuel AsanteRabi, wauzaji wa saruji, alisema hali hiyo ya bei imekuwa ikibadilika kutoka Sh. 18,000 kwa jumla hadi 19,000 kwa mfuko mmoja wa kilo 50, saruji ya Simba.

**MOROGORO**

Wakala wa mauzo ya saruji kata ya Lukobe, Manispaa ya Morogoro duka la rejareja, Zuberi Ngonyani, alisema bei ya saruji imepanda kutoka Sh. 13,500 hadi Sh. 17,000, bei ambazo wanauza kwa wateja wao kutokana na kupanda kwa gharama za ununuzi.

Naye Mariamu Abasi alisema kwa sasa anashindwa kuendelea na ujenzi kutokana na bidhaa hiyo kupanda na kuiomba serikali kuingilia kati.

Muuzaji wa jumla ya saruji, Riziki Hardware, alisema ununuzi wa saruji umepanda viwandani kwa sasa wanalazimika kuuza Sh. 13,000 hadi 16,000.

**SONGEA**

Mkoani Ruvuma mfuko mmoja uliokuwa unauzwa Sh. 14,500 sasa ni Sh. 22,000 na kulazimu wengi kusimamisha ujenzi.

Stanlei Mgaya, maarufu kwa jina la Mwanzo Mgumu ambaye ni mfanyabiashara kwenye eneo la soko kuu la Songea mjini na Somoni Mkoma, mkazi wa Lizaboni waliiomba serikali kuingilia kati.

Songea na Ruvuma wanategemea saruji kutoka katika kiwanda cha Dangote Mtwara, lakini kwa hivi sasa waliyo nayo ni ya kiwanda cha Twiga.

**DODOMA**

Mfuko mmoja umepanda kutoka Sh. 15,000 hadi Sh.18,500 kwenye maduka ya jumla huku wauzaji wa rejareja wakiuza kwa Sh. 19,500 hadi Sh. 20,500.

Akizungumza na Nipashe jana, Hamidu Msemo, ambaye ni muuzaji wa rejareja, alisema wanashindwa kumudu gharama hizo na kuhofia kupata hasara kutokana na bei kubadilika mara kwa mara.

"Mimi nina mwezi mzima sijanunua saruji kuweka dukani kwangu, na hii inatokana na kuhofia kupata hasara kwa sababu ya kushuka na kupanda kwa bei mara kwa mara," alisema Msemo.

**IRINGA**

Bidhaa hiyo imepanda kutoka Sh. 13,500 hadi 22,000 tangu mwezi Septemba.

**SHINYANGA**

Sasa mfuko mmoja umepanda kutoka Sh. 17,000 hadi Sh. 23,000, huku ikiwa adimu kwenye maeneo mengi na watu wengi kusitisha shughuli za ujenzi.

Mmoja wa wafanyabiashara Shinyanga mjini Emmanuel Mboya, akizungumza na Nipashe jana, alisema bidhaa hiyo imepanda bei kutokana na kuadimika na kwamba matofali ya saruji yamepanda kutoka Sh. 1,100 hadi 1,400.

**MWANZA**

Bei imepanda kutoka Sh. 18,000 hadi 23,000. Amosi Kazungu mkazi wa Nyamagana na Rediance Rayson mkazi wa Magu, walisema bei hiyo imewakwamisha kuendelea na ujenzi.

**TARIME WANUNUA YA KENYA**

Maeneo ya Tarime wananchi wanatumia saruji kutoka Kenya ambayo inauzwa Sh. 16,500 hadi 17,000 huku ya Tanzania ikiuzwa Sh. 24,000.

**LINDI NA MTWARA**

Inauzwa kati ya Sh. 16,000 hadi 17,000 ikiwa ni ongezeko la Sh. 3,000 hadi 4,000.

Sababu kubwa inayoelezwa ni kupungua kwa uzalishaji katika viwanda vya Dangote na Mtwara Cement.

**PWANI**

Imepanda kutoka Sh. 14,500 hadi 17,000.

**KATAVI**

Ilikuwa Sh. 20,000 sasa ni Sh. 24,000, walikuwa wakitegemea kiwanda cha Dangote, lakini imeadimika.

**MAGARI YA NJE YASOTA**

Nipashe ilishuhudia zaidi ya malori 100 yakiwa yameegeshwa kiwanda cha Wazo Hill (Twiga), Tegeta jijini Dar es Salaam, yakisubiri bidhaa hiyo.

Wakizungumza na Nipashe jana baadhi ya madereva ambao wameweka kambi kusubiri kupakia saruji hiyo kutoka Tanzania, Rwanda na Burundi, walisema kwa sasa wanalazimika kukaa hapo hata zaidi ya wiki moja.

Abdulkarim Rashid, dereva kutoka nchini Rwanda aliiambia Nipashe kuwa tangu afike nchini ana siku ya tano na hakuna dalili ya kupakia mzigo.

"Nina siku ya tano nimekuja hapa na hakuna dalili ya kupakia, kama unavyoona hata sehemu ya parking kumejaa, wote hawa wanasubiri foleni yao ifike na hatujui ni lini," alisema Rashid.

"Kipindi cha nyuma tulizoea tukifika leo, tunapakia kesho yake na kurudi nyumbani, lakini sasa imekuwa tofauti. Hii inatusababishia hasara kubwa sana kwa sababu inabidi tuingie gharama zaidi kwa hizi siku zinazoongezeka tukiwa hapa."

Mohammed Ally, alisema anatoka Kahama mkoani Shinganya na ana siku ya nane hajapata saruji.

"Hatujui kwa nini kwa sasa tunachelewa sana kupakia, ila tunaona siku hizi gari zinaingia kwa wingi kutoka nchi za jirani tofauti na kipindi cha nyuma labda huenda ndiyo sababu foleni imekuwa kubwa."

**KAULI YA SERIKALI**

Mwezi uliopita, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Riziki Shemdoe, alikwenda mkoani Tanga kuzungumza na wenye viwanda vya saruji na kuwasihi kiwango cha uzalishaji.

Alisema uzalishaji huo utasaidia kukabiliana mahitaji makubwa ya miradi kimkakati inayotekelezwa katika mikoa mbalimbali nchini. Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, serikali ipo katika mkakati wa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo kimsingi hutegemea zaidi matumizi ya saruji.

"Tusingependa kusikia visingizio vyovyote katika hilo, tunahitaji muongeze uzalishaji wa bidhaa hii, ieleweke kwamba taifa lina uhitaji mkubwa wa saruji na hatuna mpango wa kuchukua kutoka nje, tutanunua kutoka kwenye viwanda vyetu vya ndani."

**SIMBA CEMENT**

Mkurugenzi Mkazi wa Kampuni ya Simba Cement, Benny Lema, alisema kukosekana kwa umeme wa uhakika, kumepunguza kasi ya uzalishaji wa bidhaa hiyo na kusababisha kupungua kwa saruji kwenye soko la ndani.

Aliiomba serikali kuangalia upya namna ya kuviunganisha viwanda hivyo na bomba la gesi ili kuvipa uhakika wa umeme katika shughuli za uzalishaji.

**MBEYA CEMENT**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya saruji ya Mbeya, Khaled Ghareib, alisema kupanda kwa saruji kunatokana na hali ya usambazaji na uhitaji kuwa mkubwa na kushindwa kutosheleza.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Neelkanth Ltd, Amboni jijini Tanga, Rashid Lihemba, alisema awali walikuwa wakisafirisha saruji kwenda nje tani 20,000 kwa mwezi, lakini kwa sasa wanasafirisha 10,000.

"Tumesikia agizo la serikali na tulikuwa na mpango wa kuongeza uzalishaji huko siku za usoni kutoka asilimia 75 za sasa, hadi kufikia asilimia 90 ambayo ni sawa na tani 3,600 kwa siku," alisema Meneja Msaidizi wa Maweni Lime Simon Kikota.

**■Imeandikwa na Richard Makore (Mwanza), Godfrey Mushi, Allan Isack, (Arusha), Christina Mwakangale na Beatrice Shayo (DAR), Woinde Shizza (Ngorongoro), Lulu George (Tanga), Mary Mosha (Moshi), Jaliwason Jasson na Daniel Sabuni (Manyara), Christina Haule, Morogoro, Gideon Mwakanosya (Songea), Said Hamdani (Lindi), Neema Hussein (Katavi), Renatha Msungu na Ibrahim Joseph, (Dodoma), Francis Godwin (Iringa), Marco Maduhu (Shinyanga) na Julieth Mkireri (Kibaha).**

# HABARI KITAIFA



Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), Prof. Ester Dungumaro, akimkabidhi cheti mwanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari St Mary, Baswir Hood, aliyefanya vizuri masomo yote kwa ujumla kwenye mahafali ya shule hiyo, iliyopo Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, yaliyofanyika juzi. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa St Mary, Dk. Rose Rwakatare na Mwenyekiti Dallas Mhoja. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Kituo cha msaada chaomba ruzuku

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Kituo cha Msaada wa Sheria (KPC), Catherine Mlenga, amesema endapo serikali itaviwezesha kiuchumi vituo hivyo, vitafikisha elimu kwa jamii kufahamu sheria na kutambua sehemu sahihi ya kupeleka kesi zao mahali ambapo watapata msaada.

Catherine alisema kituo chao kinatakiwa kuzunguka maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Pwani, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, wamelazimika kutoa elimu katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha pekee.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi huyo alisema, wapo wanawake wananyanyasika katika ndoa na hawatambui njia za kutumia kupata haki yao, hivyo endapo kituo chao kitapatiwa ruzuku, kitafikisha elimu ya sheria katika maeneo mengi zaidi.

"Hali ya ukatili kwenye jamii zetu bado ipo na wanaonyanyasika zaidi ni wanawake na watoto. Elimu ikitolewa, itaokoa walio wengi na kupata haki zao kupitia vyombo vya sheria," alisema mkurugenzi huyo.

## Spika BLW, wajumbe wala kiapo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi (BLW) jana wamemchagua Zuberi Ali Maulid kuwa Spika wa Baraza.

Zuberi anatetea tena nafasi yake kwa kipindi cha pili kuliongoza baraza hilo.

Katika uchaguzi huo, Zuberi alipata kura 70 alizopigiwa wajumbe na wote wa baraza hilo.

Spika huyo aliwabwaga wagombea wenzake wanne, ambao wawili walikuwa pia wagombea urais wa Zanzibar katika uchaguzi uliopita wa Oktoba 28, mwaka huu.

Wagombea hao ni Hamad Mohamed kutoka Chama cha UPDP, katika uchaguzi wa uspika hakupata kura na Ameri Hassan Ameri kutoka Chama cha Demokrasia Makini ambaye alikuwa mgombea urais wa Zanzibar.

Wagombea wengine waliogombea nafasi ya uspika ni Ali Makame kutoka Chama cha CUF na Naima Salum Hamadi kutoka Chama cha UDP, ambao hawakupata kura hata moja.

Katika mkutano huo wa 10 wa Baraza la Wawakilishi, Spika wa Baraza hilo, Maulid pamoja na wajumbe wote 71 walikula kiapo cha uaminifu.

Wakati wajumbe hao 71 wakila kiapo, wajumbe wanne kutoka ACT-Wazalendo hawakuhudhuria barazani hapo.

Akizungumza baada ya kula kiapo Spika Zuberi alikipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa kumteua nafasi hiyo na kuwapongeza wajumbe wote kwa kumpigia kura na kumchagua kuendelea kuliongoza baraza hilo.

Baraza hilo lina sura nyingi mpya, wengi wakiwa vijana kutoka CCM na mmoja kutoka Chama cha ADA-TADEA ambaye aliteuliwa na Rais wa Zanzibar.


# ANATAFUTWA



115982502

**PETER JOHN MWANDIKA** ..........ANAYEONEKANA KWENYE PICHA HAPO JUU ANATAFUTWA NA POLISI KWA KESI NUMBER: **OB/RB/5054/2020** KWA TUHUMA YA WIZI WA KUAMINIWA. YEYOTE ATAKAYEMUONA POPOTE TAFADHALI TOA TAARIFA KWENYE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU YAKO.

KWA TAARIFA POLISI RIPOTI NA. **OB/RB/5054/2020.**


## JPM awashukuru waumini ujenzi wa msikiti Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. John Magufuli amewashukuru waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Imakulata, Ikulu-Chamwino, mkoani Dodoma kwa kuanzisha harambee ya kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa msikiti wa Chamwino ambao umekamilika na kuanza kutumika.

Rais Magufuli aliyeongozana na mkewe Mama Janeth Magufuli, alitoa shukrani hizo katika Misa Takatifu ya Jumapili ya 32 ya mwaka "A" iliyoongozwa na Paroko wa Parokia hiyo, Padre Paul Mapalala. Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Gerson Msigwa, ilisema Rais Magufuli aliwashukuru waumini wa madhehebu mengine ya dini waliojitokeza kuchangia ujenzi wa msikiti huo pamoja na Kanisa la Bikira Maria Imakulata Ikulu-Chamwino, ambalo ujenzi wake ulifanyika kabla, na amebainisha kuwa kitendo hicho kinadhihirisha umoja, upendo na mshikamano wa dhati walionao Watanzania.

Pia, Rais Magufuli ambaye jana alisali ibada ya kwanza ya Jumapili tangu aapishwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili, aliwashukuru waumini wa madhehebu yote ya dini kwa sala na dua zao za kuombea mchakato wa uchaguzi mkuu tangu wakati wa kampeni hadi kuapishwa kwake na amesisitiza kuwa kuchaguliwa kwake kuwa rais ni ushindi wa Watanzania wote.




## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TPLB msiwafumbie macho waamuzi 6 Simba, Yanga

**KWA** mara nyingine tena udhaifu na kukosa umakini umeonekana katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa mwishoni mwa wiki ikivikutanisha vigogo vya soka nchini, ambavyo ni watani wa jadi, Simba na Yanga.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salama na kuhudhuriwa na maelefu ya mashabiki huku Yanga ikiwa mwenyeji, ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 wafungaji wakiwa Michael Sarpong kwa aliyefunga kwa mkwaju wa penalti na Joash Onyango aliyeisawazishia Simba dakika ya 86.

Ilikuwa ni mechi iliyovuta hisia za mashabiki wengi ndani na nje ya nchi hususan kutoka mataifa ambayo klabu hizo zimesajili wachezaji wao wa kigeni, lakini mashabiki wa pande zote tambo zikiwa zimetawala kabla ya mchezo huo uliochezeshwa na waamuzi sita tofauti na watatu waliozoeleka siku zote.

Waamuzi waliochezesha mechi hiyo, wa kati alikuwa ni Abdallah Mwinyimkuu akisaidiwa na Ramadhani Kayoko, Aboubakar Mturo, Frank Komba, Mohamed Mkono na Elly Sassi.

Kwa ujumla licha ya kuwa waamuzi sita, hawakuweza kumudu mchezo huo hususan mwamuzi wa kati, Mwinyimkuu ambaye alimezea rafu nyingi bila kutoa adhabu, lakini akishindwa kwenda na kasi ya mchezo huku hata pale palipoonekana panastahili kusikiliza waamuzi wa pembeni alitoa adhabu moja kwa moja.

Nipashe ambalo limekuwa mdau mkubwa wa soka, halikufurahishwa maamuzi ya mchezo huo, ikiwamo penalti iliyotolewa moja kwa moja na mwamuzi ambayo beki Onyango alidaiwa kumchezea madhambi Tuisila Kisinda wa Yanga ndani ya eneo la hatari, wakati tukio hilo lilifanyika nje kidogo karibu na mstari wa 18. Tunaamini mshikakibendera namba mbili na aliyekuwa nyuma ya lango la Simba, walipaswa kuwa msaada mkubwa kwa Mwinyimkuu kama wangekuwa wanakwenda na kasi ya mchezo huo, lakini mwamuzi wa kati alitoa uamuzi moja kwa moja akiamini alikuwa sahihi, jambo ambalo linawafanya mashabiki na wadau wa soka kuwa na mashaka ya kuwapo kwa mchezo mchafu. Makosa aliyoyafanya si hayo, tu bali pia kuna rafu nyingi alizifumbia macho kwa pande zote mbili, ambazo zingeweza kuzua adhabu hata ya kadi nyekundu ama adhabu kama hiyo ya penalti.

Tunatangulia kusema kwamba, Nipashe si muumini wa klabu yoyote hapa nchini, kwani siku zote imekuwa ikisimamia haki michezoni kwa ujumla na kwa upande wa soka ikitaka kuona sheria 17 za mchezo huo duniani zikifuatwa bila kupindishwa ama kufinyangwa.

Ikumbukwe pia baada ya mechi ya Simba dhidi ya Tanzania Prisons iliyochezwa katika Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa kwenye ukurasa huu kolamu ya Tulonge, Nipashe liliandika kutofurahishwa na maamuzi ya mwamuzi wa kati, Shomari Lawi na kueleza udhaifu wake wa kushindwa kumudu mchezo huo.

Kama vile Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) ilisikia kilio cha Nipashe, ilipokutana Oktoba 27, mwaka huu, ilitoka na maamuzi ya kumfungia kwa kipindi cha mwaka mmoja kutokana na kushindwa kumudu mechi hiyo iliyomalizika kwa Simba kufungwa bao 1-0.

Hivyo, Nipashe ambalo Tanzania ni shabiki mkubwa wa timu zote za Taifa nchini, litaendelea kusimamia misingi na ueledi michezoni si tu haki itendeke bali ionekane ikiitendeka kweli, lengo likiwa ni kuona sekta ya michezo nchini ikikua kwa kasi na kuliletea taifa sifa stahiki lakini na kipato pia.

Tunatambua soka kama ilivyo michezo mingine ni ajira kubwa, na vijana wengi wamewekeza nguvu na akili zao huko katika kuendesha maisha yao ya kila siku, hivyo haitakuwa afya kuona juhudi zao zikikandamizwa na mtu mmoja "mwamuzi" iwe kwa makusudi, mapenzi au maslahi yake binafsi.

Ni ukweli usiopingika kuwa 'dabi' ya Simba na Yanga huvuta hisia kubwa na kufuatiliwa ndani na nje ya nchi, hivyo TPLB na TFF hawapaswi kuwavumilia ama kuwafumbia macho waamuzi kama hawa wanaolitia doa soka letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi sita, madudu yale yale, TFF wachukulieni hatua

Na Adam Fungamwango

**PAMOJA** na Bodi ya Ligi kuamua kupanga waamuzi sita kwenye mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga ili kupunguza makosa, lakini hali imekuwa tofauti.

Kwenye mechi iliyochezwa Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa kati ya Yanga na Simba, bado waamuzi hao hawakuweza kubisa kuumudu mchezo huo.

Kulikuwa na makosa mengi ya kiuamuzi na yale ambayo yangeweza kuzuilika kutokana na wingi wao. Sitoweza kuaminisha makosa mbalimbali ambayo waamuzi hao waliyafanya, lakini kwa ujumla hawakukonga nyoyo za mashabiki wengi wa soka kutokana na uchezeshaji wao.

Waamuzi waliochezesha mechi hiyo ni Abdallah Mwinyimkuu, Ramadhani Kayoko, Aboubakar Mturo, Frank Komba, Mohamed Mkono na Elly Sassi.

Wote hawa hawakuitendea haki mechi hiyo, tofauti na hata waamuzi watatu waliochezesha mechi mbili zilizopita za watani hao wa jadi.

Kwa uchezeshaji ule sikuona hata mantiki ya kuwa na waamuzi sita kwa sababu makosa tuliokuwa tukiyaona kwenye mechi zingine za Ligi Kuu yakifanywa na waamuzi watatu, ndiyo hayo hayo yaliendelea kuwatawala.

Kwa bahati mbaya sana, waamuzi wa Tanzania wanawafanya wachezaji kama maroboti ama watu wanaotumia mafuta badala ya damu kwa kuacha kufanyiana rafu mbaya, zisizokuwa na staha na za kuumizana bila kuchukua hatua yoyote jambo ambalo linanifikirisha pengine kabla ya mechi viongozi wao huwaambia "fanyeni kweli tumeshamalizana na refa".

Tangu kuanza kwa Ligi Kuu msimu huu, kumekuwa na aina fulani za rafu ambazo kwa hali ya kawaida moja tu ingefaa kabisa mtu kuonyeshwa kadi nyekundu, lakini waamuzi wamekuwa hawachukui hatua zozote.

Hii imesababisha baadhi ya wachezaji kuzoea kucheza rafu mbaya, huku wakijua waamuzi wa Tanzania wana udhaifu mkubwa kwenye kudibiti mchezo.Ninavyojua moja ya kazi ya waamuzi ni kulinda afya za wachezaji, lakini cha ajabu, mchezaji anapigwa mguu mbavuni au wa tumbo, lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa. Hii ni mbaya sana, kwani inaweza kusababisha ulemavu na kumfanya mchezaji husika asicheze tena soka wakati ndiyo kazi yake au hata kumsababishia kifo.

Kuna rafu za kawaida kabisa za kimchezo, lakini tunachoshuhudia sasa ni rafu zisizo za kiungwana kabisa na kusababisha hatari kwa mchezaji mwingine, huku waamuzi wakishindwa kabisa kuchukua hatua.

Wakati naangalia mechi ya Simba na Yanga nilishangaa kuona waamuzi wakiacha kutoa kadi hata za njano kwenye rafu mbaya, lakini wanatoa kadi za njano kwenye rafu za kawaida tu ambazo wakati mwingine hazihitaji hata kadi.

Tunaona kwa wenzetu wanavyocheza kwa tahadhari, kila mchezaji anacheza kwa kutumia kipaji na nguvu zake, rafu zozote za kuhatarisha afya za wachezaji zinachukuliwa hatua haraka na waamuzi.

Huwa tunaona si lazima mchezaji acheze rafu tatu au nne ndiyo aonyeshwe nyekundu, bali hata moja tu mbaya inatosha kabisa kumtoa mchezaji nje ya uwanja.

Na ndiyo maana tunaona wachezaji kama Ronaldo, Messi na wengine wenye vipaji wakiendelea kutamba kwa sababu waamuzi wanakuwa makini kuwalinda, dhidi ya wachezaji wenye mbinu chafu.

Nadhani kama wachezaji hao wangecheza chini ya waamuzi wa hapa, saa hizi wangekuwa wameshavunjika miguu mara mbilimbili kama si tatutatu.

Itoshe kusema waamuzi wa Tanzania, hususan wale waliochezesha mechi za Simba na Yanga wabadilike, kwani ipo siku wanaweza kusababisha hali ya uvunjifu wa amani kwa wachezaji wenyewe ndani ya uwanja, wakati mwingine hata nje.

Lakini kuna haja sasa na msimu ujao kuangalia kanuni za kuanza angalau kuagiza waamuzi kutoka nje ya nchi ili kuchezesha baadhi ya mechi za hapa nchini, hasa zile zinazoonekana ni za presha.

Tatizo ni kwamba baadhi ya waamuzi wanaochezesha mechi hizo wanakuwa na presha kuliko hata wachezaji wenyewe wanaocheza, lakini kwa dabi hiyo wakitawaliwa na mapenzi yao binafsi, hivyo kufanya makosa mengi kuliko yanayofanywa na wachezaji uwanjani.

Mfano mechi ya Jumamosi, pamoja na kusimama mara kwa mara kwa rafu zisizo na kichwa wala miguu, lakini ziliongezwa dakika mbili tu kitu ambacho mara nyingi si cha kawaida.

Hii ina maana mwamuzi tayari alikuwa na matokeo yake mkononi akihitaji sare, hivyo hakutaka kuongeza zaidi kulingana na mechi ilivyosimama, kwa kuhofia timu yoyote kupata bao.

Kwa uchezeshaji ule haikuhitaji waamuzi sita. Watatu tu wangetosha, lakini pia natarajia kuona Bodi ya Ligi (TPLB) na Shirikisho la Soka nchini zikiwachukulia hatua kwa kushindwa kumudu mechi.

# Wafanyabiashara walilia huduma ya zimamoto

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

BAADHI ya wafanyabiashara wa maduka eneo la Mji Mdogo wa Katoro mkoani Geita, wamelalamikia huduma ya zimamoto katika eneo hilo kwa muda mrefu, kitendo ambacho kinafanya maduka yao kuteketea kwa moto.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, walisema maduka mengi yameunganishwa karibu karibu, pia hakuna huduma ya zimamoto kwa muda mrefu, hivyo ni hatari kwa kuwa pindi moto unapozuka maduka na mali zao zinateketea na kurudisha nyuma maendeleo yao.

Mashaka Fabiani alisema katika tukio la moto juzi, duka lake liliteketea na mali zake zote, ingawa hajafanya tathmini kubaini hasara aliyoipata. Fabiani alisema alikuwa anauza vitu mbali mbali vikiwamo vya urembo na vipodozi.

Muhozya Mwarabu, alisema tukio hilo la moto lilitokea juzi majira ya saa 3 usiku, na kuwa kuwa wao walikuwa wamefunga maduka yao, lakini majira ya saa 3 walipigiwa siku na kuambiwa kuwa maduka yao matatu yaliteketea isipokuwa moja, ambalo haliteketea lote.

Alisema duka lililoungua ni la kijana wake, Mashaka Fabian, tukio ambalo limemsababishia hasara kubwa. Alishauri Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuongezewa vifaa vya kuokolea kwa sababu tangu tukio lilipotokea, walipewa taarifa mapema, lakini hawakuweza kufika mapema. "Gari la zimamoto lilitokea Wilaya ya Chato, lakini lilipofika halikuweza kurusha maji kwenye moto, badala yake wanachota maji kutoka kwenye gari lao na kutupia kwenye moto," alisema.

Alisema wananchi waliweza kupambana kwa kushirikiana na gari la bodoza la mtu binafsi ambalo hutembeza maji katika mji mdogo wa Katoro.

"Hilo ndilo lilisaidia sana kwa kuzima moto huo, bila gari hilo maduka yote yangeteketea," alisema.

"Tunaishauri serikali kwamba Katoro ni mji, na una wafanyabiashara wengi na ajali za moto zinatokea mara kwa mara... ingependeza sana kama wangeweza kuisogeza huduma ya zimamoto katika maeneo ya Katoro kwa ajili ya usalama kwa wananchi na wafanyabiashara wa maduka."

Aidha, alisema mji mdogo wa Katoro hauna gari la zimamoto, lipo Wilaya ya Geita na Chato.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa maduka manne ndiyo yaliyoungua.

Kamanda wa Jeshi wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Zabrone Muhumha, alisema kuwa gari la zimamoto kutoka Geita likuwa zima, lakini lilipofika eneo la tukio ghafla presha ikapungua kwa sababu maji yalikuwa kidogo, lakini zilifanyika jitihada za kuchota maji kwa kutumia ndoo kuzima moto huo pamoja na kutumia bodoza ya mtu binafsi na kufanikiwa kuzima.

# NSSF yajivunia makusanyo kuzidi kupaa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limesema makusanyo kutoka kwa wanachama yameongezeka kwa asilimia 40 kutoka Sh. trilioni 3.2 katika mwaka 2018 hadi Sh. trilioni 4.4, Juni, mwaka huu .

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa kutoa salamu za pongezi kwa Rais John Magufuli kwa kuchaguliwa tena kuongoza nchi kwa muhula wa pili, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio,

alisema chini ya uongozi wa Rais Magufuli, kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa malipo ya Serikali yaani (GePG, mabadiliko makubwa yalitokea. Alisema NSSF inatambua na kuthamini kazi kubwa iliyofanywa kwa miaka mitano iliyojaa weledi, juhudi na maarifa ikiwamo kutatua kero za wanachama.

"Tunaahidi kuendelea kuboresha huduma kwa wanachama wetu wakiwamo wastaafu wake ili wapate stahiki zao kwa wakati," alisema Erio. Shirika hilo linajivunia mafanikio makubwa ndani ya muda mfupi kutokana na usimamizi mzuri wa Bodi na Menejimenti ya NSSF, ambapo moja ya mafanikio ni kuanza kutumia GePG, hivyo kuongeza makusanyo ya kila mwezi kutoka takribani Sh. bilioni 60 hadi kufikia Sh. bilioni 100 kwa mwezi.

Erio alisema mafanikio makubwa yaliyofikiwa na NSSF katika kipindi kifupi yamechagizwa na matumizi sahihi ya GePG kwani yamewezesha ukuaji wa shirika hilo na yameongeza uwazi zaidi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**
**TASAC**

# TANZIA



MKURUGENZI MKUU WA SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC), KWA MASIKITIKO MAKUBWA ANATANGAZA KIFO CHA **NDUGU: ALLY AMANI CHOMY,** KARANI MSAIDIZI KILICHOTOKEA ALFAJIRI YA TAREHE 06 NOVEMBA, 2020 KATIKA HOSPITALI YA DAR-GROUP JIJINI DAR ES SALAAM.

MKURUGENZI MKUU KWA NIABA YA BODI NA MENEJIMENTI ANATOA SALAM ZA POLE KWA FAMILIA, WAFANYAKAZI WA TASAC NA WOTE WALIOGUSWA NA MSIBA HUU.

HAKIKA ATAKUMBUKWA KWA **"UCHAPAKAZI, UADILIFU NA UZALENDO KATIKA KIPINDI CHOTE CHA UHAI WAKE".**

***TUNAWAOMBEA WOTE FARAJA NA SUBIRA NJEMA KATIKA KIPINDI HIKI KIGUMU CHA MAJONZI. MUNGU AILAZE ROHO YA MAREHEMU MAHALI PEMA PEPONI.***

**AMINA**

**Imetolewa na;**

**MKURUGENZI MKUU**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC).**

**Jengo la PPF Tower, Sakafu ya 7 na 8, Kiwanja Na. 20/21, Mtaa wa Garden/Ohio, S. L. P. 989, Dar es Salaam - Tanzania, Simu: +255 222 127 314, Nukushi: +255 222 127 313, Barua Pepe: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz, Tovuti: www.tasac.go.tz**

# Rais Mwinyi amteua Makamu wa Pili wa Rais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amemteua Hemed Suleiman Abdallah, kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, alisoma barua kutoka Ikulu ambayo ilisomeka kuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amefanya uteuzi wa jina la Hemed Suleiman Abdallah kushika wadhifa wa kiutendaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Nimepokea barua kutoka Ikulu ambayo inalitaja jina la Hemed Suleiman Abdallah kuwa makamu wa pili wa rais wa Zanzibar," alisema Maulid baada ya hapo vifijo na shangwe zilitawala kutoka kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walioshangilia uteuzi huo na kuahirishwa shughuli za baraza hadi kesho.

Suleiman ambaye ni mzaliwa wa kisiwani Pemba, Jimbo la Mkoani aliwahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi ikiwamo ya ofisa katika Wizara ya Fedha ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika ofisi ziliopo Pemba na kupanda ngazi hadi ofisa mdhamini wa Wizara ya Biashara na Viwanda.

Mwaka 2015 alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Mkoani Pemba, ambapo baada ya miaka miwili alipanda ngazi na kuteuliwa kuwa mkuu wa mkoa wa Kusini Pemba.

Mapema Suleiman alikula kiapo cha mjumbe wa Baraza la Wawakilishi baada ya kuteuliwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kupitia nafasi kumi.




Meneja wa Kiwanda cha Konyagi, Aranyaeli Ayo (kulia), akikata utepe kuzindua mchezo wa bahati ya mawakala wa kampuni hiyo, uliofanyika jijini Dar es Salaam, mawakala 4 kila mmoja alijishindia pikipiki za matairi 3. Kushoto kwake ni Meneja Usimamizi wa Kanda wa Mauzo wa TDL, Mwesige Mchuruza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto aagiza wanasheria sakata la katibu mkuu

**Na Elizabeth Zaya**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema wamewaagiza wanasheria wao kuhakikisha wanafuatilia na kuhakikisha Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Zanzibar, Nassor Mazrui, anafikishwa mahakamani haraka.

Zitto alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tumewaagiza wanasheria wetu wafuatilie na kuhakikisha kwamba Mazrui na wenzake wote ambao wanashikiliwa na Jeshi la Polisi ama waachiwe au wafikishwe mahakamani," alisema Zitto. "Tunafahamu kwamba kuna taratibu za kisheria ambazo zinajulikana baada ya polisi kuthibitisha kuwa wanaye, kwa hiyo tumeomba hatua za haraka zifanyike, au afikishwe mahakamani haraka au aachiwe,"

Katika mkutano huo na waandishi wa habari, Zitto alisema ameandika barua kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola akimtaka achunguze kwa kina matukio yaliyotokea katika uchaguzi mkuu wa Tanzania.

"Na baada ya kufanya uchunguzi, washirikiane na Umoja wa Afrika kusimamia uchaguzi mpya Tanzania," alisema Zitto.

Kadhalika, alisema ameandika barua kwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kumtaka aunde timu ya viongozi wastaafu wa Afrika walioheshimika na pia kuteua watu wanaotokana na tume huru za uchaguzi katika nchi mbalimbali za Afrika ili zisimamie uchaguzi mpya ambao alidai kwamba unapaswa kufanyika Tanzania.

Zitto alisema chama chake hakikubaliani na matokeo ya uchaguzi uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu nchini.

# Askofu Gavile aishukuru serikali kuokoa uhai wake

**Na Francis Godwin,** IRINGA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Iringa, Blaston Gavile, aliyekuwa amelazwa chumba cha uangalizi maalum (ICU), Hospitali ya Taifa Muhimbili, ameipongeza serikali chini ya Rais Dk. John Magufuli kwa kuboresha huduma za afya nchini na kuokoa maisha yake.

Askofu Gavile, aliyeambatana na viongozi wa majimbo, alitoa kauli hiyo jana, wakati akitoa salamu kwa waumini wa kanisa hilo Usharika wa Kanisa Kuu Iringa, baada ya kurejea kutoka katika matibabu. Alisema, alipatwa na tatizo la kuugua ghafla akiwa Chimala mkoani Mbeya na baadaye alikimbizwa katika Hospitali ya Rufani Mbeya na kisha kupelekwa Muhimbili ambako alifikia ICU na kote huduma za afya zilikuwa ni nzuri zenye kuridhisha.

"Nalazimika kuja kwenu leo kusema asante kwa wema wenu waumini wote wa kanisa hili hapa Iringa, Mbeya na Dar es Salaam kipindi chote nikiwa ICU mlinifariji sana japo mimi nilikuwa nimekata tamaa ya kuishi kiasi cha kuagiza rafiki zangu kuitazama familia yangu, pia napenda kuishukuru sana serikali imehusika kunusuru uhai wangu kutokana na huduma nzuri za afya katika hospitali zetu," alisema askofu Gavile.

"Huduma nzuri za afya, hata madaktari na wahudumu katika hospitali wamefanya kazi kwa moyo wa kujituma zaidi kiasi cha Watanzania wanaofika kupatiwa huduma za matibabu kuwa na imani zaidi tofauti na zamani." Alisema ili serikali iendelee kutekeleza majukumu yake vyema, Watanzania wote kwa imani zao hawana budi kuendelea kuwaombea viongozi akiwamo Rais Dk. John Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya kuwatumikia Watanzania.

## Wazazi washauriwa kukatia bima watoto

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI nchini wameshauriwa kuwakatia bima ya elimu watoto wao, ili waendelee na masomo hata mzazi wake anapopata majanga.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 11 ya Shule ya Sekondari ya Ghome. Alisema benki hiyo imejikita kuendeleza sekta ya elimu kupitia huduma nafuu na za uhakika hasa katika kugharamia masomo.

"Tumebuni huduma hizi ili kuwa na mpango wa kudumu pale ambapo yanatokea majanga kama vile kifo au ulemavu wa kudumu, kuhakikisha watoto wanaendelea kupata elimu stahiki," alisema.

Benki hiyo imebuni bidhaa na huduma za kibenki ambazo zinatoa fursa kwa wazazi na walezi kuwapa watoto elimu bora ambayo ni msingi mkubwa wa maendeleo katika ngazi ya familia na kitaifa.

"Kupitia akaunti ya Chanua, wazazi wanaweza kuweka akiba kwa ajili ya kugharamikia ada za kwa urahisi zaidi na kwamba pia huduma ya bima ya elimu inampa mzazi uhakika hata pale anapopata matatizo ikiwamo kifo au ulemavu."

Alisema benki hiyo ina mpango wa kuwaendeleza wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kuwapa udhamini (Scholarship) na kwa mwaka 2019/2020 jumla ya wananfunzi 63 wamenufaika na mpango huo jambo linaloongeza fursa ya upatikanaji wa elimu.

"Tunaitazama sekta ya elimu kama sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na vilevile kiuchumi, NBC tumewekeza jitihada katika kubuni bidhaa na huduma mbalimbali ambazo zitawawezesha wazazi na walezi kuwapa watoto wao elimu bora na ya uhakika," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Ghome, Ivon Mbieli, alisema moja ya maeneo ambayo taasisi hiyo imejikita ni kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora ili kuweza kuleta matokeo chanya kwenye jamiii na taifa kwa ujumla.

"Tuna imani kubwa wanafunzi hawa wataendelea na elimu za juu zaidi na baadaye waje kuwa wataalamu mbalimbali kwa manufaa ya taifa letu," alisema mkuu huyo.

HABARI KITAIFA

# Mawasiliano ya barabara sasa yarejeshwa Mtwara

**Na Thereza Chimagu**

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) umefanikiwa kufanya ukarabati wa barabara iliyoharibiwa na mvua na kusababisha kukatika kwa mawasiliano kati ya Vijiji vya Libobe na Ming'wena vilivyopo Kata ya Libobe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara mkoani humo.

Akizungumzia ujenzi wa barabara hiyo, Meneja wa TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Mhandisi Patrick Kanyagha, alisema baada ya kupata changamoto ya kukatika kwa barabara hiyo waliomba fedha za dharura kutoka TARURA Makao Makuu na kupatiwa shilingi milioni 185 ambazo zilitumika kutengeneza barabara iliyopo kati ya Kijiji cha Libobe hadi Ming'wena yenye urefu wa kilomita 4.8, kwa kiwango cha changarawe ili wananchi waendelee na shughuli zao za kiuchumi.

"Kipande hiki ni sehemu ya barabara ya Libobe - Ming'wena - Likwidi - Mtama yenye jumla ya urefu wa Km 19, na tulichukua maamuzi ya kutengeneza baada ya mvua kuharibu miundombinu ya barabara pamoja na kuathiri makazi ya wananchi, ili kurejesha mawasiliano na kuwezesha wananchi kusafirisha bidhaa zao kama hapo awali," alisema Mhandisi Kanyagha.

Meneja huyo alisema baada ya kupatiwa fedha hizo, kazi walizozipa kipaumbele zilikuwa ni kurejesha tuta, kujenga "box culvert" mpya ambapo zimejengwa nene, kujenga mtaro wa maji ya mvua na kurejesha tabaka la changarawe urefu wa kilomita 3.5, ambapo kazi zote zimekamilika na mawasiliano yamerejea katika vijiji hivyo.

Naye Majid Rashid, mkazi wa Kijiji cha Ming'wena, aliipongeza serikali kwa kutengeneza barabara katika eneo hilo kwani imesaidia kupunguza kero ya usafiri na kufanya wananchi waendelee na shughuli zao kama hapo awali. "Tunaishukuru TARURA kwa kutujali na kutufanyia ukarabati wa haraka kwani tulikuwa na changamoto ya usafiri kutoka hapa hadi kufika barabara kuu ya Mpapora kwani magari na hata pikipiki yalikuwa hayapiti kabisa, lakini baada ya matengenezo ya barabara tumefaidika sana na imerahisisha mawasiliano," alisema Rashid.

Naye Somoe Kankunje, mkazi wa Kijiji cha Ming'wena, alisema upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii katika eneo hilo umerahisishwa na ukarabati wa barabara hiyo kwani hawapati shida ya usafiri na wanaendelea na biashara zao kama awali bila matatizo.

TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara inaendelea na kazi mbalimbali, zikiwamo za matengenezo ya barabara na vivuko katika wilaya hiyo, ili kuwawezesha wananchi kusafiri na kusafirisha mazao pamoja na bidhaa zao kwa urahisi.



Naibu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) anayeshughulikia taaluma, utafiti na ushauri, Dk. Prosper Mgaya (kushoto), akipeana mikono na Mkufunzi wa IATA kutoka Houston Texas, Marekani, Andre Aurelien, baada ya kozi fupi ya IATA jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: PROSPER MAKENE**

# IATA yanoa wakufunzi viwango vya kimataifa

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji kimewawezesha wakufunzi kupata mafunzo ya kozi fupi kutoka Shirika La Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (IATA).

Mafunzo hayo yalikuwa ni ya wiki sita kuwajengea uwezo wakufunzi na pia wakufunzi kukidhi ubora wa viwango vya kimataifa.

Miongoni mwa wakufunzi wa Chuo waliopata mafunzo hayo ni pamoja na marubani kutoka Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), Precision Air, Wakala wa Ndege wa Serikali, Mamlaka ya Usafiri wa Anga na wahadhiri kutoka Shule Kuu ya Teknolojia ya Usafiri wa Anga ya NIT.

Kozi zilizosomwa na wakufunzi hao kuanzia Septemba 28 hadi Novemba 04 ni Mfumo wa Usimamizi wa Ubora wa Unga, Mbinu za Kufundisha, Mfumo wa Usimamizi wa Usalama wa Anga, Makosa ya kibinadamu, Ukaguzi katika masuala ya Anga pamoja na Usimamizi wa Rasilimali na Utekelezaji katika Anga.

Hadi kumaliza kozi zote sita, wataalamu wa anga wapatao 150 wamenufaika na mafunzo haya yaliyotolewa hapa NIT. Haya ni mafanikio makubwa sana katika kuhakikisha mafunzo ya taaluma ya anga yanaendeshwa katika ubora unaokidhi viwango vya kimataifa.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye hafla ya kufunga mafunzo kwa kozi ya wakufunzi hao katika Kampasi Kuu ya NIT Mabibo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Shule ya Teknolojia ya Usafiri wa Anga, Denis Mwageni, alisema:

"Kwa sasa wakufunzi wetu wana uelewa mpana wa maeneo yote yaliyofundishwa ambayo pia ni muhimu sana kwa mujibu wa sheria na taratibu za Mamlaka ya Usafiri wa Anga ili kuweza kuendesha kozi za anga kwa ufanisi zaidi."

"NIT tayari ni kituo cha IATA kilichoruhusiwa kufundisha kozi nne fupi za usafiri wa anga ambazo ni; Airline Marketing, Airline Customer Service, Airport Operations Fundamentals, global distribution systems fares na ticketing-Amadeus. Kozi hizi zitaanza kufundishwa mwaka huu wa masomo (2020/21) katika kampasi ya NIT Mabibo," alisema.

Mwageni alisema kozi za IATA wanazoanza kuzitoa ni fursa kwa Watanzania wote kwa sababu watazipata NIT kwa gharama nafuu, na pia kupata fursa ya ajira katika mashirika ya ndege ya ndani na kimataifa.

Alielezea kuwa lengo la chuo ni kuongeza kozi zaidi za IATA ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka katika sekta ya anga inayokua kwa kasi nchini.

"Mbali na kuanza kutoa kozi za IATA, NIT pia imepanga kuanza kutoa shahada ya kwanza ya uhandisi wa matengenezo ya ndege na stashahada ya uhandisi wa matengenezo ya ndege pamoja na kozi fupi za uhandisi mwaka huu ili kuwaanda wahandisi wasio na leseni waweza kufanya mitihani ya leseni," alisema.

Mkufunzi wa IATA kutoka Houston Texas, Marekani Andre Aurelien, aliwaambia wakufunzi waliopata mafunzo hayo kuwa jambo kubwa la kuzingatia katika sekta ya anga ni usalama kwanza.

Kwa upande wake, Naibu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma Utafiti na Ushauri, Dk. Prosper Mgaya, alisema: "Tunaziomba kampuni za ndege za ATCL, Precision Air na kampuni zingine kuleta hapa wafanyakazi wao kuja kusoma kozi hizi zilizoidhinishwa na IATA, kwani zitawasaidia katika kukuza na kuendesha vyema kampuni zao."

Mmoja wa waliohudhuria mafunzo hayo, Kapteni Hilal Fuad, kutoka Shirika la Ndege Tanzania - ATCL alisema NIT imefanya uamuzi mzuri sana kuanza kutoa kozi za IATA, kwa sababu zinatoa maarifa ya kina na ufahamu mkubwa katika tasnia ya anga. Kozi hizi zinakuongezea utaalamu zaidi.

# Wafanyabiashara wafagilia kukutanishwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UMOJA wa wafanyabiashara ambao ni wateja wa Benki ya NMB katika mikoa ya Shinyanga, Geita na Tabora (Business Club's), umeipongeza benki hiyo kwa kuweka utaratibu wa kukuta na wateja wao na kuwasikiliza.

Wafanyabiashara hao wamesema kuwa kuwa kupitia utaratibu huo, imekuwa fursa kubwa kwao kuelezea changamoto ambazo zimekuwa zikiwakabili katika biashara zao ikiwa pamoja na kutoa maoni ya kuboreshwa kwa huduma za benki hiyo.

Wafanyabiashara hao wakiwamo wajasiriamali, kutoka katika wilaya za Kahama mkoa wa Shinyanga, Mbogwe Mkoa wa Geita na Uyui Tabora, walisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kukutanishwa na benki hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wenyeviti wa umoja huo, Mwenyekiti wa Business Club kutoka Wilaya ya Kahama, Azan Said, alisema kuwa utaratibu huo wa kukaa pamoja na wateja wake unawapa nguvu ya kuendelea kufanya kazi na benki hiyo.

Saidi aliongeza kuwa kupitia utaratibu huo ambao uwasilisha changamoto zao, maoni na ushauri imewafanya kuwa imara katika biashara zao na kusababisha wawe warejeshaji wazuri wa mikopo wanayochukua kwa wakati.

Naye Haji Nasoro mfanyabiashara alisema wameendelea na kulizishwa na maboresho ya huduma yanayoendelea kufanywa na NMB, ambapo aliwataka wafanyabiashara wengine kuchangamkia fursa zinazotolewa na benki hiyo.

"Benki ya NMB imekuwa mkombozi kwa muda mrefu kwetu, kupitia utaratibu huu wa kukutana, tumefanikiwa kunufaika kwa kiwango kikubwa kwani huduma nyingi zimeboreshwa hasa katika mikopo ya kibiashara," alisema Nasoro.

Katika kongamano hilo Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, aliwahakikishia wafanyabiashara hao kuwa benki hiyo itaendelea kuweka mazingira mazuri zaidi katika kuwawezesha kiuchumi ili kwenda na wakati na ukuaji wa uchumi wa taifa.

Magesse alisema wamekuwa na utaratibu wa kukaa na wateja wao kila mwaka, lengo likiwa kuboresha huduma na nini wanachotaka benki ifanyie katika kukua kiuchumi.

"Benki yenu ya NMB inamilikiwa na wateja kwa hisa zenu pamoja serikali na inahakikisha huduma za kibenki zinawafikia popote mlipo kupitia mawakala wetu na kwa umuhimu huo, ndiyo maana inaendelea kuyafanyia kazi mawazo na ushauri wao," alisema Magese.

# Akutwa na kesi ya kujibu madai kubaka mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita Mkoa wa Geita, imemkuta mkazi wa Bukondo Nestory Nkola (19), kuwa ana kesi ya kujibu baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wake.

Uamuzi huo mdogo ulitolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Sosthenes Kiiza, baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi.

Kiiza alisema mshtakiwa huyo anakabiliwa na kosa moja la kubaka msichana mwenye umri wa miaka 16 ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mapinduzi.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alipeleka mahakamani mashahidi wanne na vielelezo vitatu.

Hakimu Kiiza alisema mwathirika wa tukio hilo, alithibitisha mahakamani kuwa mshtakiwa ni mpenzi wake na kudai kuwa baba wa binti huyo aliwakuta mshtakiwa na binti yake wakiwa ndani wakifanya mapenzi, na kwamba baada ya tukio hilo baba wa binti huyo alitoa taarifa kituo cha polisi na mshtakiwa huyo akakamatwa.

Alisema upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo na mahakama imemwona mshtakiwa ana kesi ya kujibu.

Mshtakiwa huyo alidai mahakamani kuwa atajitetea kwa kiapo hana shahidi.

Hakimu Kiiza aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 25, mwaka huu kwa ajili ya mshtakiwa huyo kutoa utetezi wake.

Aidha, alisema mshtakiwa ataendelea na dhamana yake hadi tarehe iliyopangwa kwa ajili ya kutoa utetezi wake.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alidai kuwa tarehe isiyofahamika kati ya Januari na Machi 8, mwaka huu, katika Kijiji cha Bukondo Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimbaka msichana mwenye umri wa miaka 16 ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mapinduzi.




Ofisa Biashara Mkuu wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts, akiwa kwenye gari la CRDB Wakala kuashiria uzinduzi rasmi wa kampeni ya "Tupo Mtaani Kwako", ambayo inalenga kuhamasisha matumizi ya huduma za benki, kutoa elimu juu ya masuala ya fedha, pamoja na kuwaunganisha Watanzania kutumia huduma za benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhakiki wa maeneo ya wazi waendelea

**Na Mwandishi Wetu,** SUMBAWANGA

OFISI ya Ardhi Mkoa wa Rukwa, inaendelea na utaratibu wa kufanya uhakiki wa maeneo ya wazi na maeneo ya umma yaliyoorodheshwa kwa mujibu wa ramani za mipango miji za halmashauri za mkoa huo.

Lengo la utaratibu huo ni kubaini kama kuna uvamizi umefanyika katika maeneo hayo.

Akizungumzia kuhusiana na utekelezaji wa mpango huo, Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Rukwa, Swagile Msananga, alisema kuwa lengo la kutekeleza mpango huo ni kupata orodha kamili ya maeneo ya wazi ili yaweze kutambulika rasmi, huku akiwaonya wananchi waliovamia katika maeneo hayo.

"Kwa maeneo ambayo yatakuwa yamevamiwa, hakutakuwa na namna ya kufanya, isipokuwa wavamizi wataondolewa ili kupisha maeneo ya wazi kwa sababu yanatakiwa yalindwe kwa nguvu zote.

"Na maeneo ambayo yapo salama mpaka sasa, tutahakikisha mipaka yake inawekwa wazi na wananchi watatakiwa waiheshimu," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya kupata orodha kamili ya maeneo hayo atakabidhiwa mkurugenzi, ili aweze kuyaandalia hati kwa ajili ya ulinzi wa maeneo hayo kwa siku za usoni.

## CRDB yazindua kampeni ya kuhamasisha wananchi

**Na Nelson Simon,** SAUT

BENKI ya CRDB imezindua kampeni ya 'Tupo Mtaani Kwako' inayolenga kuhamasisha matumizi ya huduma za kibenki na kuwaunganisha Watanzania walio wengi kutumia huduma zake.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Biashara Mkuu wa Benki hiyo, Dk. Joseph Witts, alisema kampeni hiyo itasaidia kuelimisha wateja juu ya fursa mbalimbali wanazozitoa.

"Tuna jukumu la kuhakikisha tunasaidia kuboresha maisha ya Watanzania kupitia bidhaa na huduma zetu na kampeni hii tunakwenda kutimiza wajibu huu kwa kutembelea mtaa kwa mtaa Tanzania nzima kuhakikisha wananufaika na fursa zinazotolewa na CRDB," alisema.

Dk. Witts alisema CRDB imejipanga kuwatembelea wateja waliko ofisini, sokoni, dukani, stendi na kuwapatia huduma.

"Tutakuwa tukitumia magari na mabango ambayo tutayaweka mtaani kwa ajili ya kusogeza huduma kwa wateja," alisema.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo inalenga kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utoaji huduma ikiwamo CRDB Wakala, SimBanking, TemboCard na Internet-Banking.

Alisema kupitia njia hizo, mteja anaweza kufanya miamala yake ya kibenki popote alipo kwa urahisi, usalama na unafuu.

Meneja wa Kanda ya Mashariki ya Benki ya CRDB, Badru Idd, aliwataka Watanzania kuchangamkia fursa hiyo na kuahidi kuwa benki hiyo imejipanga kikamilifu kuhakikisha inamfikia kila mtu.

"Tunaanza na Kanda ya Mashariki ambayo inajumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar na baadaye kusambaa nchi nzima. Niwaombe Watanzania wanapoona wafanyakazi wetu mtaani, wasisite kuuliza maswali na kuja kupata huduma, hii ni benki yao na tupo tayari kuwahudumia," alisema.

Nipashe
Spotika



WAKALI 10 WA MABAO LIGI YA MABINGWA ULAYA UK. 12-13



Winga wa Simba, Luis Miquissone, akichezewa madhambi na Kiungo wa Yanga, Tuisila Kisinda katika mechi ya dabi iliyochezwa Uwanja wa Mkapa juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAMBO 7 USIYOYAJUA 'DABI' SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE 'dabi' ya Kariakoo iliyochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ilimalizika kwa timu hizo kufungana bao 1-1, shukurani kwa bao la kusawazisha la Joash Onyango dakika tano kabla ya mechi kumalizika lililoifanya Simba kuponea chupuchupu kuadhirika.

Awali, Yanga ilikuwa imepata bao kwa mkwaju wa penalti ya Michael Sarpong dakika ya 31, baada ya penalti tata iliyotokana na Tuisila Kisinda kudaiwa kuangushwa eneo la hatari na Onyango, ingawa marudio ya picha za video yanaonyesha kuwa ilikuwa nje kidogo ya mstari wa 18.

Lilikuwa ni pambanao kali la kukata na shoka, ambalo timu ziligawana vipindi, Yanga ikiinyanyasa Simba kipindi cha kwanza na Simba iliipelekesha Yanga kipindi cha pili. Kama kawaida mechi za 'dabi' huwa zina mambo mengi, zikiwamo rekodi, takwimu kutoka kwa timu zenyewe au wachezaji.

Baada ya mechi hiyo ya kiporo cha raundi ya saba ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mwandishi amekusanya rekodi na takwimu mbalimbali za 'dabi' hiyo na zilizopita pia, twende sasa...

### #1. MECHI YA NNE MWAKA HUU

Ilikuwa ni mechi ya nne kwa mwaka huu wa 2020, tatu zikiwa ni za Ligi Kuu na moja ya Kombe la FA. Katika mechi hizo, kila timu imeshinda mara moja na sare mbili. Mechi ya kwanza ya mzunguko wa kwanza Ligi Kuu msimu uliopita iliyochezwa Januari 4, mwaka huu, timu hizo zilitoka sare ya bao 2-2, na mechi ya mzunguko wa pili msimu uliopita iliyochezwa Machi 8, mwaka huu, Yanga ilishinda bao 1-0, huku mechi iliyochezwa Julai 13 ya Kombe la FA hatua ya nusu fainali, Simba ikishinda mabao 4-1, kabla ya sare ya Jumamosi.

### 2. WAFUNGAJI WOTE WA 'DABI' NI WAGENI

Licha ya kwamba wafungaji wa mabao yote si wazawa, lakini ni mara yao ya kwanza kucheza mechi ya 'dabi' ya Kariakoo. Sarpong, raia wa Ghana ni mara yake ya kwanza kucheza, kwani alisajiliwa msimu huu akitokea Rayon Sports ya Rwanda.

Kwa upande wa Onyango ambaye ni Mkenya, alisajiliwa msimu huu akitokea Gor Mahia ya Kenya, hii ikiwa pia ni mara yake ya kwanza kucheza dabi hiyo.

### 3. SARE YA KWANZA YA 1-1 TANGU 2017

Hii ni sare ya kwanza ya bao 1-1 tangu mwaka 2017. Mara ya mwisho timu hizo kufungana bao 1-1 ilikuwa Oktoba 28, 2017 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Simba ikipata bao kupitia kwa Shiza Kichuya dakika ya 57, kabla Obrey Chirwa hajasawazisha dakika tatu baadaye, ikiwa ni Ligi Kuu msimu wa 2017/18.

Baada ya hapo timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana Septemba 30, 2018, ligi ya msimu wa 2018/19 na 2-2, Januari 4, mwaka huu, ligi ya msimu uliopita.

### 4. ONYAGO AWEKA REKODI YA NYONI

Onyango amekuwa beki wa kwanza kufunga bao kwenye mechi ya Simba dhidi ya Yanga tangu mwaka 2018. Beki huyo wa kati alifunga bao kwa kichwa akiunganisha nyavuni mpira wa kona iliyopigwa na Luis Miquissone na kuweka rekodi iliyowekwa na Erasto Nyoni Aprili 29, 2018.

Ilikuwa ni Ligi Kuu msimu wa 2017/18 beki huyo wa kati alipofunga bao dakika ya 37 akiunganisha faulo iliyopigwa na Kichuya.

### 5. SARPONG, MGHANA WA TATU KUFUNGA DABI

Sarpong anaweka rekodi ya kuwa mchezaji wa tatu kutoka nchini Ghana kufunga bao kwenye mechi za watani wa jadi Simba dhidi ya Yanga. Wachezaji wote ni wakiitumikia Yanga.

Wengine ni Benard Morrison aliyefunga bao Machi 8, mwaka huu, Yanga ikiifunga Simba bao 1-0, na Kenneth Asamoah aliyefunga bao Julai 10, 2011 kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Kagame mwaka 2011, Yanga ikishinda bao 1-0 na kutwaa ubingwa.

### 6. ONYANGO, MKENYA WA NNE KUFUNGA DABI

Onyango amekuwa mchezaji wa nne kutoka Kenya kufunga mabao kwenye mechi za dabi, na wa pili kwa Simba.

Wachezaji wengine ni Mosses Odhiambo wa Simba kwenye mechi iliyochezwa Julai 8, 2007, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1, mwingine akiwa ni Ben Mwalala wa Yanga akifunga dabi mara mbili Oktoba 26, 2008 bao pekee Yanga ikishinda 1-0, lingine akifunga Aprili 19, 2009, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2.

Hilary Echessa wa Simba yeye alifunga bao kwenye michuano ya Kombe la Kagame, Yanga ikiifunga Simba mabao 2-1 na 2010, alifunga bao la nne, Simba ikiichapa Yanga mabao 4-3.

### 7. MECHI YAISHA BILA 'OFFSIDE'

Ni mechi iliyoisha bila timu yoyote kuotea, huku kila timu ikipata kadi tatu za njano, Simba ikifanya madhambi mara 20 na Yanga mara 16. Yanga ilipata kona tisa, wakati Simba ilifanikiwa kupata kona tano. Yanga ilipiga mashuti manne yaliyolenga lango na matatu ambayo hayakulenga, huku Simba ikipiga mashuti mawili tu yaliyolenga na manane ambayo yalitoka nje.

## ISIKUPITE

EDINSON Cavani (miaka 33 na siku 267) amekuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga bao kwenye mechi yake ya kwanza Ligi Kuu England tangu Zlatan Ibrahimovic alipofanya hivyo Agosti 2016 (wakati huo akiwa na umri wa miaka 34 na siku 316). Cavani alifunga bao hilo juzi kwenye Uwanja wa Goodison Park wakati United ikishinda 3-1 dhidi ya Everton.



Extra Time

# WAKALI 10 WA MABAO LIGI YA MABINGWA ULAYA



RONALDO

**NYON,** Uswisi

MICHUANO ya Ligi ya Mabingwa Ulaya imeshuhudia wachezaji bora kizazi na kizazi na wengi wao wakifunga mabao ya kuvutia na kujiwekea rekodi zao.

**Makala haya yanakuchambulia wachezaji 10 ambao wamefunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika kizazi cha sasa, hawa hapa...**

### #10. LUIS SUAREZ - ATLETICO MADRID | MABAO 30

Luis Suarez amejiimarisha yeye mwenye kama mmoja wa washambuliaji bora wa kiazazi chake, shukrani kwa miaka sita aliyokaa pale Barcelona, ambako alishinda Kiatu cha Dhahabu kwa kuwa mfungaji bora Ulaya msimu wa 2015-16.

Akiwa na mabao 198 pale 'Blaugrana', kwa sasa anashika nafasi ya tatu kwa kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo na pia ndiye mfungaji bora wa timu ya Taifa ya Uruguay akiwa na mabao 62 kwenye mashindano yote.

### #9. EDINSON CAVANI - MANCHESTER UNITED MABAO 35

Edinson Cavani kama ilivyo kwa Suarez, amekuwa na mafanikio makubwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na akitamba zaidi pale kwa waajiri wake wa zamani, Paris Saint-Germain.

Cavani mara zote anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote kwa PSG alitua hapo akitokea Napoli, ambako alifunga mabao 104 katika mechi 138 na pia akiwa na Paris Saint-Germain, alifunga mabao 200 kwenye mechi 301.

Sasa akiwa anacheza pale Manchester United anaweza kuongeza idadi ya mabao yake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #8. NEYMAR - PARIS SAINT-GERMAIN | MABAO 35

Alishinda mataji matatu msimu wa 2014-15 akiwa na Barcelona, Neymar anaungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Paris Saint-Germain, Cavani akiwa amefunga mabao 35 kwenye Ligi ya Mabingwa katika misimu saba.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, hivi karibu alifikia rekodi ya Ronaldo Nazario kwa kufunga mabao mengi katika timu ya Taifa ya Brazil akiwa na mabao 62 kwenye mchezo wa kuwania kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Peru.

### #7. SERGIO AGUERO - MANCHESTER CITY| MABAO 46

Sergio Aguero ni mchezaji pekee kutoka Ligi Kuu ya England katika orodha hii akiwa anacheza pale Manchester City. Raia huyu wa Argentina amekuwa bora zaidi katika kufunga mabao kwa Man City akifunga 255 katika mechi 372, na kwenye Ligi ya Mabingwa hadi sasa ametikisa nyavu mara 46.

### #6. THOMAS MULLER - BAYERN MUNICH | MABAO 46

Thomas Muller mara kwa mara amekuwa akielezewa kama mmoja wa washambuliaji waliokamilika zaidi duniani, hasa kutokana na uwezo wake wa kufunga mabao. Alishinda tuzo ya mfungaji bora kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2010 na amefunga zaidi ya mabao 200 kwa Bayern Munich.

### #5. ZLATAN IBRAHIMOVIC - AC MILAN | MABAO 49

Zlatan Ibrahimovic amefurahia mafanikio mengi akicheza katika ligi saba tofauti duniani, na amekuwa akifunga mabao mengi ya kuvutia.

Hata hivyo, anabaki kuwa mmoja wa wachezaji wakubwa kama Gianluigi Buffon ambao hawajawahi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alishinda taji la Ligi ya Europa akiwa na Manchester United mwaka 2017. Msimu huu pia anacheza kwenye mashindano hayo akiwa pale AC Milan, lakini ana rekodi ya kutikisa nyavu mara 49 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #4. KARIM BENZEMA - REAL MADRID | MABAO 65

Karim Benzema ni mmoja wa wachezaji wenye mafanikio makubwa katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Na ni mmoja wa washambuliaji aliyeshinda taji hilo mara nyingi zaidi.

Akiwa na mabao 65, alishinda mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid chini ya kocha Zinedine Zidane.

### #3. ROBERT LEWANDOWSKI - BAYERN MUNICH | MABAO 68

Robert Lewandowski amekuwa mmoja wa wachezaji ambao kiwango chake hakijawahi kushuka, huku msimu bora zaidi kwake ni ule wa 2019-20, ambapo alifikisha mabao 50 kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Straika huyo wa zamani wa Borussia Dortmund alifunga mabao 55 katika mashindano yote msimu uliopita na kutwaa Kiatu cha Dhahabu Ulaya. Pia alikuwa kinara wa mabao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na mabao 15 wakati miamba hao wa Bavaria wakitwaa kombe hilo.

Alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa msimu wa 2019-20 na ameendelea na kasi ile ile msimu huu wa 2020-21 akiwa tayari amepachika mabao 10 katika mechi 10 tu alizocheza za Bundesliga.

Kwenye Ligi ya Mabingwa anashika nafasi ya tatu kama mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi (68) na ana nafasi ya kuongeza zaidi msimu huu.

### #2. LIONEL MESSI - FC BARCELONA | MABAO 116

Lionel Messi ni mmoja kati ya wachezaji wawili tu waliofikisha zaidi ya mabao 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nyota huyu wa Barcelona amepitwa na Cristiano Ronaldo pekee kwa kuwa na idadi ya mabao mengi kwenye michuano hiyo ya Ulaya akifunga 116 katika mechi 144. Messi ambaye ni mshindi mara sita wa Ballon d'Or ana nafasi ya kufunga zaidi mabao kwenye mashindano hayo msimu huu.

### #1. CRISTIANO RONALDO – JUVENTUS | MABAO 131

Ukizungumzia Ligi ya Mabingwa Ulaya, Cristiano Ronaldo anabaki kuwa ndiye mfalme wao.

Nyota huyu wa kimataifa wa Ureno ana rekodi nyingi zaidi katika mashindano hayo na jina lake linajulikana vizuri sana.

Amefunga mabao 131 kwenye mashindano hayo akiwa katika Klabu za Manchester United, Real Madrid na Juventus, mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote. Bado anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwa msimu mmoja, wakati alipotikisa nyavu mara 17 msimu wa 2013-14 akiwa pale Real Madrid.


Msimu huu anaweza kuifikia rekodi ya Clarance Seedorf ya kubeba taji hilo akiwa na klabu tatu tofauti.

## Nukuu

"Wakati natua England, Arsenal ilikuwa timu ngumu sana ikiwa na Gilberto Silva na viungo wakubwa, hivyo ilikuwa timu ngumu kucheza nayo. Lakini nadhani Arsenal niliyocheza nayo kuelekea mwisho wa taaluma yangu kisoka ingeweza kufanya hivyo ikiwa na mchezaji kama Thomas Partey, namjua vizuri, imefanya usajili mzuri," **kiungo wa zamani wa Chelsea, Michael Essien.**



"Mimi sina tatizo kuitwa jina lolote, hata wewe [mtangazaji] wanaweza kukuita dada, vyovyote watakavyo, ila babu hawezi kuwafunga," **beki wa Simba, Mkenya Joash Onyango akizungumzia kuitwa babu na mashabiki wa Yanga, baada ya juzi kuifungia timu yake bao la kusawazisha dhidi ya watani zao hao.**



"Bila shaka kama si yeye ni mwingine, ni kuhusu ushindani. Kurt Zouma ambaye anafanya vizuri kule Chelsea anaijua vizuri timu ya Taifa ya Ufaransa. Mlango haujafungwa. Nimefanya uchaguzi huo leo kwa sababu maalumu. Na inaweza kuwa hivyo hivyo kwa Machi na Juni? **Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps akizungumzia kutomuita beki Dayot Upamecano.**






# KLABU 5 ZA EPL ZILIZOTUMIA FEDHA NYINGI USAJILI 2020

**LONDON, England**

BAADA ya uvumi mwingi wa usajili, hatimaye dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto lilifungwa rasmi Oktoba 5, mwaka huu.

**Klabu za Ligi Kuu zimekuwa zikitumia fedha nyingi kwenye usajili na zote 20 kwa ujumla wake zilitumia pauni bilioni 1.24 kipindi hicho cha usajili wa majira ya joto.**

Klabu kama Chelsea, kwa mfano zimetumia fedha nyingi wakati wa usajili kwa kusajili wachezaji saba chini ya utawala wa kocha, Frank Lampard pale Stamford Bridge.

Makala haya inaziangalia klabu tano ambazo zimetumia fedha nyingi zaidi kwenye usajili kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2020, hizi hapa...

**#5. ARSENAL | PAUNI MIL. 64.5**

Arsenal ya kocha Mikel Arteta ilikuwa na hatari ya kukosa kumsajili mchezaji mkubwa katika dirisha hilo. Zikiwa zimesalia saa kadhaa kabla ya dirisha kufungwa, 'Washikabunduki' hao wakafanikisha usajili wa Thomas Partey wa pauni milioni 45 kutoka Atletico Madrid.

Usajili wa nyota huyo wa kimataifa wa Ghana ulikuja wakati tayari Arsenal ikiwa imeshawanasa Willian na Gabriel Magalhaes kwa pauni milioni 27.

Arsenal pia ilijikuta ikiwaachia wachezaji wengi kuondoka akiwamo Henrikh Mkhitaryan, Matteo Guendouzi, Lucas Torreira na mwengineo. Hata hivyo, wakati hao wengine wakiwa wameachiwa kwa mkopo, ni Emi Martinez pekee ndiye aliyeweza kuiingizia fedha Arsenal alipouzwa kwa Aston Villa kwa pauni milioni 17.

**#4. MANCHESTER CITY | PAUNI MIL 76.5**

Manchester City walitajwa kama ambao wangefanya usajili wa kufuru katika dirisha hilo, baada ya kuachia taji la Ligi Kuu kwenda Liverpool tena kwa tofauti ya pointi 18. Walijikuta kwenye wakati mgumu baada ya kuumia kwa Aymeric Laporte na kuondoka kwa Leroy Sane.

Walijaribu kuziba mapengo yao kwa kuwasajili, Nathan Ake na Ferran Torres mwanzoni mwa dirisha la usajili kwa pauni milioni 41 na pauni milioni 20.8. Baadaye kulikuwa na uvumi mwingi kuhusu usajili wa mlinzi wa kati na Pep Guardiola akafanikiwa kumsajili Ruben Dias wa SL Benfica kwa pauni milioni 65.

Hata hivyo, kuondoka kwa Sane, ambaye ametua kule Bayern Munich baada ya kuwa na mafanikio makubwa hapo Manchester. Uhamisho wake wa pauni milioni 54.8 pamoja na kuuzwa kwa Nico Otamendi kwa pauni milioni 13.7 kukaiwezesha City kurudisha fedha zake zaidi ya nusu walizotumia kwenye usajili wa kipindi hicho.

**#3. LEEDS UNITED | PAUNI MIL. 84.5**

Baada ya kukosekana kwenye Ligi Kuu ya England kwa karibia miaka 16, Leeds United ilitengeneza historia kwa kushinda kule Daraja la Kwanza na kupanda Ligi Kuu. Kikosi hicho cha Marcelo Bielsa kikaingia kwenye usajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake.

Leeds ilivunja rekodi yake ya usajili kwa kumchukua nyota wa kimataifa wa Hispania, Rodrigo Moreno kwa pauni milioni 27. Pia wakamsajili kwa fedha ndefu Diego Llorente kutoka Real Sociedad kwa pauni milioni 20 na pia straika wa Brazil, Rafinha kutoka Rennes kwa pauni milioni 17.

Lakini kikosi hicho cha Bielsa kikawatoa wachezaji wenzake kadhaa. Walimwachia moja kwa moja Helder Costa aliyekuwa anacheza kwa mkopo kule Wolves.

**#2. ASTON VILLA | PAUNI MIL. 85**

Kuwapo kwa Aston Villa kwenye orodha hii kunaweza kuwashangaza wengi, hasa kutokana na ukweli kwamba, walikaribia kushuka daraja msimu uliopita. Kikosi hicho cha kocha, Dean Smith kililazimika kuingia sokoni ili kuimarisha timu yao pale Villa Park.

Ikiwa imeingia kwenye mwaka wake wa pili kwenye Ligi Kuu baada ya kupanda, Villa iliamua kusajili wachezaji wenye ubora tu.

Wakanunua wachezaji kama Matty Cash (pauni milioni 16) kutoka Nottingham Forest, kipa Emi Martinez (kwa pauni milioni 17) kutoka Arsenal, straika wa Olympique Lyon, Bertrand Traore (kwa pauni milioni 19) na wakavunja rekodi yao ya usajili kwa kumsajili, Ollie Watkins, ambaye alitua hapo kwa pauni milioni 33 kutoka Brentford. Pia wanapata huduma ya Ross Barkley anayecheza kwa mkopo wa muda mrefu.

**#1. CHELSEA | PAUNI MIL. 212.6**

Nani ambaye alitarajia Chelsea itaongoza kwenye orodha hii? Blues walijiwekea rekodi ya kufanya usajili wa wachezaji saba. Kikosi hicho cha Lampard kilifungiwa kufanya usajili baada ya kuvunja sheria ya usawa wa fedha za ununuzi wa wachezaji majira ya joto yaliyopita.

Hivyo, wakaamua kurudi sokoni kwa nguvu na kasi kubwa na Lampard akatengeneza machaguo kadhaa.

Edouard Mendy (kwa pauni milioni 22), Hakim Ziyech (pauni milioni 33.3), Timo Werner (pauni milioni 45), Ben Chilwell (pauni milioni 50), na pengine usajili wa fedha nyingi zaidi tangu walimpomnunua Eden Hazard mwaka 2012.

Kai Havertz (pauni milioni 75.8) kutoka Bayer Leverkusen – wote kwa ujumla wao walitumia kiasi cha pauni milioni 200. Kwa nyongeza wakamchukua mkongwe kutoka PSG, Thiago Silva na Malang Sarr kwa usajili huru.

**JE, WAJUA?**



PIERRE-EMERICK Aubameyang ni mchezaji wa kwanza Arsenal kuweza kuzamisha penalti kimyani kwenye Uwanja wa Old Trafford katika mechi za Ligi Kuu England, hakuna penalti yoyote iliyozamishwa nyavuni na mchezaji kutoka Gunners kati ya zilizopigwa kipindi cha hivi karibuni uwanjani hapo na (Robin Van Persie mwaka 2011 na Gilberto Silva mwaka 2006).



# Wafugaji waomba maduka ya serikali dawa za kuku

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAFUGAJI wa kuku mkoani Dodoma, wameiomba serikali kuanzisha maduka ya kuuza dawa za mifugo kwa wingi ili kuwaondolea adha ya kununua kwa bei ghali kwenye maduka binafsi.

Katibu Mkuu wa kikundi cha Tupendane cha watu wenye ulemavu kinachojishughulisha na ufugaji wa kuku, Bashiru Kajuna, alitoa ombi hilo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Kajuna alisema kuwa pamoja na halmashauri na jiji kutoa mikopo yao kwa wana vikundi mbalimbali vya ujasiriamali, bado wafugaji wakiwamo wa kuku, wanakabiliwa na tatizo la bei kubwa kwenye dawa za mifugo katika maduka binafsi hali inayosababisha wengi wao kutomudu gharama hizo na kushindwa kufuga.

"Hivyo tunaiomba serikali ianzishe maduka hayo kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo vijijini, wilayani hadi mkoani ili kurahisisha upatikanaji wake, lakini kuwapo kwa bei rahisi itakayosaidia wafugaji kujiinua kiuchumi na kufikia malengo yao ya ufugaji wa kuku.

"Ni imani yetu serikali kama ilivyokusudia kwa kupitia halmashauri pamoja na majiji ambayo imekuwa ikitoa mikopo hiyo ya kuwainua watu wake kiuchumi, wataliangalia hilo kwa jicho la pili la kufungua maduka hayo ambayo yataondokana na bei kubwa iliyopo kwenye maduka binafsi," alisema.

Aliomba wajasiriamali kuheshimu maelekezo yanayotolewa na halmashauri pamoja na jiji kwenye mikopo wanayopewa ikiwamo kurudisha kwa wakati ili watu wengine wapate fursa ya kukopeshwa.

Alisema mikopo inayotolewa ni muhimu ikaheshimiwa kwa wajasiriamali kwa kuwa ni mkombozi katika kuwatatulia tatizo la umaskini.

"Vikundi vizingatie sheria, kanuni na taratibu kama zinavyoelekeza, pia tusigeuze mitaji kuwa anasa, kwa kuwa wajasiriamali wakifanya hivyo watasababisha kukwamisha jitihada za serikali za kuwakwamua kiuchumi," alisema.

Alisema kuwa wengine wamejikuta wakifilisika kutokana na kutumia mikopo hiyo kinyume na malengo.



Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, akizungumza na baadhi ya wafanyakazi wa wizara hiyo, kwenye mafunzo ya kiutendaji yaliyofanyika mwishoni wa wiki jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CCT yajipanga kukomesa ukatili kijinsia

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JUMUIYA ya Kikristo Tanzania (CCT), imejipanga kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto katika mikoa mitatu nchini ambayo ni Dodoma, Singida na Mara.

Akizungumza jana kwenye kongamano la wajane na wagane lililoandaliwa na Jumuiya hiyo, Mratibu wa Idara ya Maendeleo ya Wanawake, Watoto na Jinsia, Esther Muhagachi, alisema wamejipanga kutokomeza ukatili kwa kutoa elimu kwenye mikoa hiyo.

"Huu mkakati wa utoaji elimu utaendelea katika mikoa mingine tunataka kuhakikisha wanawake na watoto wanajua haki zao za msingi," alisema.

Alisema elimu hiyo ni muhimu kwa kuwa kuna baadhi ya wazazi wanakatiza ndoto za watoto wao kielimu kwa kuwaozesha wakiwa na umri mdogo jambo ambalo ni ukatili kwa watoto hao.

Alisema matukio ya aina hiyo yamekuwa yakichangia kwa kiasi kikubwa kurudisha nyuma maendeleo ya watoto hasa wa kike. Kadhalika, Muhagachi alisema wanampango wa kuanzisha klabu za kupinga ukatili wa kijinsia katika shule za msingi na sekondari ambazo zitasaidia kutoa elimu kwa wanafunzi kujua haki zao za msingi kielimu.

Alisema wanaamini klabu hizo zitasaidia kuwajengea uwezo wanafunzi wa kutambua haki zao za msingi hususani wakiwa shuleni. "Klabu hizi ni muhimu kuanzishwa kwa sababu zitasaidia wanafunzi kutoa taarifa pale wanapokutana na matukio ya ukatili wa kijinsia," alisema Muhagachi.

Naye Askofu wa Kanisa la Mungu Tanzania, Boniface Msupha, aliwapongeza CCT kwa kuandaa kongamano hilo ambalo linasaidia kuyakumbusha makanisa namna ya kusaidia wagane na wajane.

Alisema wagane na wajane nao ni watu wa muhimu kama ilivyo kwa wengine.

Askofu Msupha alisema uzinduzi wa kampeni ya sauti ya ushindi ikatumike ipasavyo ili isaidie kufanikisha kusudio la kongamano hilo la wajane na wagane.

Hata hivyo, aliwakumbusha viongozi wa dini kuendelea kuwakumbuka wajane na wagane kwa kuwatunza bila kuteswa.

Alisema pamoja na serikali kuwatetea, lakini makanisa yanapaswa kuwapa kipaumbele wajane na wagane wasiwe wanyonge. Kwa upande wake, Askofu wa kanisa la Amazing Grace, Paul Mwanga, alisema kongamano hilo liwe chachu ya makanisa kuendelea kukumbuka kutoa msaada kwa wajane na wagane.

Askofu Mwanga alisema kila mmoja anajukumu la kusaidia watu hao, hivyo ni vyema makongamano kama hayo yafanyike ili kusaidia kuikumbusha jamii kuendelea kuwakumbuka wajane na wagane.

# Bodi yaagizwa uvunaji, uhifadhi maji ya mvua

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

BODI ya Maji ya Taifa imeagizwa kuandaa mkakati wa kitaifa wa uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Anthony Sanga, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifungua kikao cha 13 cha Bodi hiyo, jijini hapa.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na mvua nyingi ambayo ikitumika vizuri itaongeza upatikanaji wa maji nchini na kuondokana na tatizo la uhaba wa maji.

"Naiagiza Bodi ya Maji kufanya haraka iwezekanavyo kuja na mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha maji ya mvua tunayazuia ili yasipotee, watu wa rasilimali maji wanasema maji hayapotei kwa sababu yanakwenda ardhini, lakini yapo ambayo yanaishia baharini, hata hayo yanayokwenda chini ya ardhi bado tunampa ugumu mwananchi kuyafikia na kuyavuna," alisema.

Alisema mikakati mikubwa imefanyika kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa na hivyo nguvu kwa sasa inapaswa kuelekezwa katika uanzishwaji na uendelezaji wa mabwawa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Taifa, Prof. Hamisi Nkotagu, alisema bodi hiyo imepokea agizo hilo na imepanga kulijadili kwa upana katika kikao kijacho ili kushauri wizara hiyo.

Alisema katika kikao kijacho ataitwa mtaalamu wa maji aliyebobea eneo la rasilimali maji ili wajadiliane na kupata njia sahihi ya utekelezaji suala hilo.

"Tumepokea maagizo yako Katibu Mkuu, maji ya mvua yanapoenda baharini yanakuwa yamepotea kabla hayajaenda baharini tunaweza kuyakinga tukaweka mabwawa madogo ambayo jamii itatumia," alisema.

"Sisi bodi pamoja na watu wa mabonde ya maji ambao tumekutana hapa tumekubaliana mkutano ujao tuwe na mtaalamu aliyebobea katika masuala haya atushauri na tuwe na kauli moja ya kuishauri serikali."





# Wadau waweka mpango mkakati ukatili wa kijinsia

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WADAU wa masuala ya ukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Mbeya, wameweka mpango mkakati katika kukabiliana na vitendo hivyo ili jamiii iendelee kuwa salama.

Wakizungumza jana kwenye kikao cha kujadili na kuweka mkakati wa kutokomeza vitendo hivyo ambacho kilihusisha Mahakama, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jeshi la Polisi na Idara ya Maendeleo ya Jamii walisema ni wakati muafaka wa kupaza sauti.

Mratibu wa Kituo cha Wasaidizi wa Kisheria Mbeya (MBEPACE), Laiki Ndagile, alisema kuwa lengo la mpango huo ni kutokomeza vitendo hivyo ambavyo ni vya ubakaji, ulawiti na vipigo.

Alisema licha ya wanawake na watoto kuwa wahanga hayo kuna tatizo la watu hao kutotoa taarifa wanapofanyiwa vitendo vya kikatili.

"Kuna changamoto kubwa ya vitendo vya ukatili wa kingono kwa wanawake na watoto mbaya zaidi hawatoi ushirikiano kwa Jeshi la Polisi, wanawakumbatia watuhumiwa kutokana na mahusiano waliyonayo kwenye familia zao naomba tubadilike," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Anna Gloria Gereta, alisema hospitali hiyo imekuwa ikipokea watoto wengi ambao wanafanyiwa vitendo vya kikatili.

Alisema miongoni mwa vitendo vinavyoripotiwa ni ulawiti kwa watoto wa kiume na wa kike na kwamba wanapohitaji ushirikiano kutoka kwa wazazi wanakosa.

Alisema licha ya hospitali hiyo kupokea watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo, alidai mpango mkakati huo waliokubaliana katika kikao hicho utaleta tija kwani wataendelea kutoa elimu kwa kuwashirikisha wazazi na walezi.

Aliongeza kuwa wananchi wanaendelea kupata elimu dhidi ya vitendo vya ukatili katika Mkoa wa Mbeya kwani vinaendelea kupungua.

# Wafugaji Mbarali wapewa siri ya kuepuka migogoro ya ardhi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

WAFUGAJI katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameshauriwa kununua ardhi kwa ajili ya kuchungia mifugo yao badala ya kutegemea maeneo yaliyotengwa na serikali, ili kuondokana na migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, ambaye aliwataka wafugaji hao kuacha tabia ya kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha matukio ambayo yanasababisha migogoro ya mara kwa mara ikiwamo mapigano miongoni mwao. Alisema maeneo yaliyotengwa na serikali hayatoshelezi mahitaji kutokana na baadhi ya wafugaji kufuga mifugo mingi na hivyo kufanya maeneo yaliyotengwa na serikali kutokidhi mahitaji.

"Mfugaji ambaye umeamua kufuga mifugo mingi, muanze kununua ardhi yenu ili majani yanapokauka ama kuisha kwenye maeneo yaliyotengwa na serikali muyatumie maeneo yenu," alisema Chalamila. Awali baadhi ya wafugaji walimweleza Mfune matatizo yanayowakabili ikiwamo uhaba wa maeneo ya kuchungia, huku wakiomba serikali kulifuta Tangazo lake namba 28 la mwaka 2008 (GN 28) ambalo lilipanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na hivyo kupunguza maeneo ya kuchungia. Mmoja wa wafugaji hao, Shaban Olelenganu, ambaye ni mfugaji wa Kijiji cha Mwanavala, alisema kijiji hicho kina eneo la wafugaji ambalo lilipimwa wakati wa uwekaji wa matumizi bora ya ardhi, lakini limevamiwa na wakulima.

Alisema hali hiyo imewafanya wafugaji kukosa maeneo ya kuchungia na kwamba wakitaka kuchungia katika eneo hilo inaibuka migogoro na wakulima ambao alidai ndio wavamizi.

"Sisi wafugaji tunakuwa kama hatuhitajiki katika wilaya hii, watu wa TANAPA wanatuzuia kuchungia kwenye hifadhi, wakulima nao wamevamia eneo letu, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa na serikali," alisema Olelenganu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbarali, Hashim Mwaliaga, aliomba serikali kusaidia kufikisha kilio cha wananchi wa wilaya hiyo, ili mipaka ya hifadhi irekebishwe. Alisema GN 28 ndio chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi katika wilaya hiyo kwa maelezo kuwa imechukua maeneo mengi ya wananchi wilayani humo na kuyafanya kuwa sehemu ya hifadhi.



Mwandishi wa Chama cha Habari za Utalii na Uwekezaji Tanzania (TAJATI), Ulimboka Mwakilili, akiangalia chanzo cha maporomoko ya maji Nhumbi kilichopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Kituo maalum usambazaji wa teknolojia chaanzishwa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imeanzisha kituo maalumu cha usambazaji wa teknolojia na maarifa ya kilimo bora kwa wananchi, ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Kituo hicho kipo katika viwanja vya maonyesho ya wakulima (Nanenane) vya John Mwakangale jijini Mbeya na kitafanya kazi kwa mwaka mzima, huku kukiwa na vipando vya mazao mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema elimu itakuwa inatolewa kwa nadharia na vitendo katika eneo hilo na kwamba mashamba ambayo huwa yanatumika kwenye maonyesho ya Nanenane ndiyo yatatumika.

Alisema jengo la taasisi hiyo ambalo hutumika wakati wa maonyesho ya Nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ndilo litakuwa linatumika kama darasa la kuwafundishia wananchi nadharia za kilimo kabla ya kuwapeleka shambani kujifunza kwa vitendo.

Dk. Bucheyeki alisema waliamua kuanzisha kituo hicho ili kuwasaidia wananchi ambao huwa wanakosa nafasi ya kuhudhuria maonyesho hayo, ambayo huwa yanafanyika kwa muda wa siku nane pekee.

"Kuna wataalamu wa kutosha ambao tumewahamishia hapa, watakuwa wanafanya kazi muda wote katika eneo hili, eneo hili lipo ndani ya taasisi yetu kwa hiyo itakuwa rahisi wananchi kujifunza hapa na hata kulekule kituo kikuu," alisema Dk. Bucheyeki.

Msimamizi wa kituo hicho, Lusungo Paul, alisema mpaka sasa kituo hicho kimeanza kupokea watu mbalimbali ambao wanaenda kujifunza wakiwamo wanafunzi wa vyuo mbalimbali vya kilimo.

Alisema walengwa wa kunufaika na kituo hicho ni wakulima mmoja mmoja, vikundi vya wakulima, mashirika ya umma na binafsi, mikoa na halmashauri za mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na wadau wengine wa kilimo.

Paul ambaye anatoka katika Idara ya Usambazaji wa Teknolojia na Uhusiano wa TARI, alisema kituo hicho kitakuwa kinatumika kama wakala wa kusambaza teknolojia zinazozalishwa na taasisi hiyo na kwamba kipo jirani na kituo cha mabasi cha Nanenane na hivyo ni rahisi wananchi kukifikia.

"Tunaziomba mamlaka za serikali za mitaa hasa wakurugenzi wa halmashauri na hata taasisi zisizokuwa za serikali ziwalete wananchi kuja kujifunza teknolojia hapa ili wazalishe kwa tija na kuinua uchumi," alisema Paul.





# Vikwazo vita dhidi ya udhalilishaji watoto hivi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA wa Ustawi wa Jamii Zanzibar, Mkasi Abdullah Rajab, amesema kuwa kuna vikwazo mbalimbali vya kimalezi na kijamii vinavyojitokeza na kuchangia udhalilishaji wa watoto Zanzibar.

Alisema miongoni mwa vikwazo hivyo ni uwajibikaji mdogo wa wazazi, walezi na familia katika kuwasimamia na kuwafuatilia watoto, mienendo yao, ratiba zao na marafiki wanaokuwa nao.

Hayo yalielezwa wakati akiwasilisha mada ya malezi ya watoto katika mkutano wa waandishi wa habari kuhusu malezi mbadala kwa watoto uliofanyika juzi Mjini Zanzibar.

Alisema kikwazo kingine ni wazazi na walezi kutokuwa karibu na watoto wao na kuzungumza nao kuhusiana na masuala mbalimbali ya stadi za maisha na mabadiliko ya kimwili na kihisia kwa mujibu wa umri na hatua za ukuaji wa watoto.

Alieleza kuwa pia muhali katika familia na jamii katika kuyaibua matukio ya udhalilishwaji ambayo yanaathiri saikolojia ya watoto, maendeleo yao na malezi kwa ujumla.

Aidha, alieleza kikwazo kingine ni kukithiri kwa talaka na kutengana kwa wazazi na familia, ushirikiano mdogo kati ya wazazi na walimu wa shule na madrasa katika kufuatilia maendeleo ya watoto kimasomo.

"Katika suala la malezi, familia na jamii ina sehemu kubwa ya kuwaweka watoto kwenye mazingira salama kwa kukinga madhara yasitokee kwa watoto na kuchukua hatua," alisema.

Aliongeza kuwa: "Kukithiri kwa talaka na kutengana kwa wazazi na familia, hali inayosababisha ushirikiano mdogo kati ya wazazi na kuwaweka watoto kwenye mazingira hatarishi."

Naye Nyezuma Issa, mratibu wa mradi wa malezi mbadala kwa watoto kutoka kijiji cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (SOS), aliwataka walezi waliojikubalisha kubeba jukumu la malezi kwa watoto wanaohitaji malezi mbadala kuwajibika ipasavyo na kuwaweka watoto kwenye mazingira mazuri.

Alisema kuwa mradi wa malezi mbadala kwa awamu ya pili, watoto 100 kutoka vijiji vya Donge Kipange, Mtowapwani na Pale watanufaika ambao watoto hao wanaishi katika mazingira magumu.

Alisema miongoni mwa watoto hao wengi ni yatima na wengine wametelekezwa na wazazi wao, hali ambayo imesababisha kuishi katika mazingira hatarishi.

Mwanasheria kutoka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto, Didas Khalfan, aliwataka waandishi wa habari kuandika habari za uchunguzi kuhusu udhalilishaji wa watoto.

Alisema kuwa waandishi wa habari wasiishie kuripoti tu matukio ya udhalilishaji, badala yake kufuatilia kesi hizo hadi mwisho wa hukumu.



Mwenyekti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, akiangalia picha ya X-ray ya mmoja wa wafuasi wa chama hicho, ambao waliathirika kupigwa na watu wasiojulikana katika harakati za uchaguzi mkuu wa mwaka huu, Visiwani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mwinyi ateua wanne Baraza la Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefanya uteuzi wa wajumbe wanne wa Baraza la Wawakilishi, ambapo kwa mujibu wa sheria, Rais huwa na nafasi kumi za uteuzi kwa wajumbe wa baraza hilo.

Amefanya uteuzi huo kwa mujibu wa uwezo aliopewa chini ya kifungu namba 66 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Aliowateua juzi ni Sada Mkuya Salum ambaye alishawahi kuwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kipindi cha uongozi wa Rais mstaafu Jakaya Kikwete.

Mwingine ni Juma Ali Khatib, ambaye alikuwa mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ADA-TADEA na pia alikuwa waziri mstaafu wa wizara isiyokuwa na wizara maalum katika Serikali ya Zanzibar ya awamu ya saba.

Yumo pia Tabia Maulid Mwita ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana wa CCM (UVCCM) Taifa.

Mwingine ni Hemed Suleiman Abdallah ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba.

Rais wa Zanzibar, anatarajia kuteua Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na Makamu wa Kwanza, ambapo kwa mujibu wa sheria ndani ya siku saba baada ya Rais kula kiapo hutakiwa kuteua viongozi hao.

Wakati Rais anatarajiwa kufanya uteuzi huo, bado Chama cha ACT-Wazalendo kinaendelea na vikao vyake vya ndani vya kujadili iwapo wataingia au kutoingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa mujibu wa sheria, chama kilichopata asilimia 10 kitaungana na chama kilichopata ushindi kuunda serikali hiyo. ACT-Wazalendo ndiyo iliyofikisha asilimia hiyo.

# Wajumbe 14 wa viti maalum Baraza la Wawakilishi watajwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imewatangaza wajumbe 14 kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa nafasi ya viti maalum vya wanawake vya ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Akitangaza majina ya wajumbe hao juzi, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Hamid Mahmoud, alisema wajumbe 18 ni CCM kwa mujibu wa masharti na maelekezo ya ibara ya 67 ya katika ya Zanzibar ya mwaka 1984. Alisema tume imewatangaza wajumbe hao baada ya kuridhika kuwa wote wana sifa ya kuwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Zanzibar ibara ya 68.

Waliotangazwa na ZEC ni Panya Ali Abdallah, Bihindi Hamad Hassan, Salma Mussa Bilali, Shadya Moh'd Suleiman, Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba), Sada Ramadhan Mwenda na Mwantatu Mbaraka Khamis.

Wengine ni Zainab Abdallah Salum, Riziki Pemba Juma, Leila Muhamed Mussa, Salha Mwinyi Juma, Hudhaima Mbarak Tahir, Sabiha Fil fil Thani, Aza Januar Joseph, Mwanaid Kassim Mussa, Mgeni Hassan Juma, Mwanajuma Kassim Makame na Rahma Kassim Ali. Tume imeshawasilisha majina ya wajumbe hao kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya hatua nyingine za kisheria.

# Umuhimu uzalishaji malighafi ya saruji wahimizwa nchini

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema kuzalishwa kwa malighafi ya kutengeneza saruji nchini itasaidia kupunguza gharama kubwa iliyokuwa ikitumika kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Hazina Ndogo jijini Dar es Salaam, Evance Bernard, wakati akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango katika uzinduzi wa ofisi ya kampuni ya saruji ya Mbeya.

Alisema kampuni hiyo imefanya jambo la muhimu kwa kuanza kutengeneza malighafi za kuzalisha saruji badala ya kuagiza nje ya nchi itasaidia kuokoa gharama kubwa.

Bernard alisema serikali ina hisa ya asilimia 25 kwenye kampuni ya saruji ya Mbeya na wameweza kusaidia sekta ya viwanda.

"Tunawapongeza kwa kuwa na ofisi Dar es Salaam na kuzalisha bidhaa mpya hapa nchini itapunguza gharama kubwa ya uagizaji kutoka nje ambayo ilikuwa inatumia fedha nyingi," alisema Bernard.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo, Khaled Ghareib, alisema mkakati wa kampuni hiyo ni kuongeza uzalishaji kulingana na mahitaji ya sasa ya bidhaa hiyo.

Alisema kuanza kuzalisha malighafi za kutengeneza saruji nchini itawasaidia kupunguza gharama pamoja na kuongeza kiwango cha uzalishaji.

Ghareib alisema miaka ijayo wanatarajia kuongeza kiwango kikubwa cha uzalishaji na kusambazwa kwa wingi sokoni.

Alisema Tanzania inaagiza nje ya nchi wastani wa tani 40,000 za malighafi ambazo hutumika katika sekta ya ujenzi.

Alisema kampuni hiyo inamiliki hisa asilimia 65, serikali asilimia 25 na Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) asilimia 10.



Balozi wa Vodacom Tanzania Foundation, Laurent Edward (kushoto), akitoa elimu ya programu ya Vodacom Instant Schools (Soma Kidijitali) kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Puge, Nzega Tabora kupitia mpango huo utamwezesha mtumiaji kupata masomo, kutafuta na kupakua maudhui mbalimbali kwa njia ya mtandao bila gharama yoyote. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu magonjwa mlipuko kupungua Maswa zaanikwa

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mji Mdogo wa Maswa mkoani Simiyu, imefanikiwa kupambana na kupunguza kwa kiwango kikubwa kasi ya magonjwa ya mlipuko, hususani kipindupindu katikati ya mji.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Afya wa Mamlaka hiyo, Saimon Nyadwera, alisema mafanikio hayo yametokana na usimamizi mzuri wa sheria, kanuni za mazingira pamoja na utoaji wa elimu.

Alisema licha ya wilaya hiyo kutenga siku ya Jumamosi ya kila wiki kufanya usafi nyakati za asubuhi, lakini wakazi wa mji huo wamekuwa na utamaduni wa kufanya usafi wa mazingira yao kila siku.

"Tabia ya kuchukia uchafu na kutunza mazingira ambayo imejengeka katika jamii yetu ya wananchi wa mji wa Maswa ni jambo zuri, na wameonekana kuheshimu sheria ya mazingira na kanuni zake kwa hiari, ni kitu muhimu katika kulinda na kutunza mazingira, afya za watu na viumbe wengine," alisema Nyadwera.

"Sisi Idara ya Afya ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Maswa katika kipindi cha miaka mitano tumetoa elimu kupitia vyombo vya habari na kuandaa mikutano mbalimbali ya wadau wa mazingira na wananchi kwa ujumla wake na tumepata mafanikio makubwa kwa kuwa takwimu zinaonyesha magonjwa ya milipuko kama kipindupindu, kasi ya kuenea kwake imepungua sana, hatujakumbana na kipindupindu miaka mitano iliyopita."

Pia, alisema kuwa mafanikio hayo yamepatikana kutokana na ushirikiano mkubwa walioupata kutoka kwa wananchi kupitia kwa viongozi wa dini, viongozi wa serikali za mitaa na halmashauri ya wilaya hiyo ya Maswa.

Alisema watahakikisha wanaendelea kusimamia kanuni na sheria za mazingira ili kuendelea kudhibiti magonjwa ya milipuko katika mji huo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyonge, alisema kutokana na mwitikio chanya ya wananchi wa eneo hilo amepanga kumwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kuunda timu ambayo itakuwa na kazi ya kuhakikisha matatizo yote ya kimazingira yanashughulikiwa haraka.

Kaminyoge pia aliwaonya baadhi ya wenye viwanda vidogo na wananchi katika mji huo wanaoendelea kutitirisha maji machafu kuacha mara moja tabia hiyo na kwamba watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

# Manispaa Morogoro ilivyopania kuwa jiji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, ameuagiza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Manispaa ya Morogoro kuandaa mpango wa haraka wa kutengeneza barabara zote za lami zilizoharibika ndani ya manispaa hiyo.

Alisema hayo mjini hapa wakati wa uzinduzi wa stendi ya daladala ya Kaloleni iliyopo Kata ya Mji Mpya Manispaa ya Morogoro.

Aliwataka wakazi wa manispaa hiyo kutunza miundombinu iliyopo kwenye maeneo yao ikiwamo ya barabara na stendi za kisasa iliyojengwa kwa kutumia ya fedha nyingi za serikali ambazo zinatokana na kodi zao.

Msulwa alisema njia moja wapo ya kuthamini fedha zao ni kulinda miundombinu iliyopo na inayoendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali ndani ya wilaya hiyo.

Alisema lengo la halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ni kuwa jiji, hivyo ni lazima miundombinu iweze kuboreshwa licha ya kuwa zipo changamoto zitakazojitokeza.

Msulwa alisema hatuwezi kukaa katika manispaa kwa miaka 32 na kuendelea kukaa kwa muda mrefu kabla hatujafikia kiwango cha kuwa Jiji.

"Napongeza hatua ambazo manispaa imezichukua zinatufanya kuelekea kuwa Jiji, nafahamu ipo stendi kuu ya daladala Mafiga, soko kuu la kisasa, na miradi mingine ambayo inaendelea... wahandisi wa miradi mnafanya kazi kubwa na nzuri," alisema Msulwa.

Katika hatua nyingine, Msualwa aliahidi kutoa Sh. milioni moja kwa ajili ya kuchangia mfuko wa fedha za ukarabati wa kituo kidogo cha Polisi cha Mji Mpya kilichopo eneo la standi hiyo ili kutoa huduma bora kwa jamii.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Michael Waluse, alisema uongozi wa manispaa hiyo utashirikiana na uongozi wa daladala katika stendi ya Kaloleni katika masuala mbalimbali.

Waluse alisema baada ya ukarabati wa stendi hiyo na kuongeza miundombinu ikiwamo vyoo vya kisasa kutawezesha kuongeza makusanyo kutoka wastani wa Sh. 30,000 hadi 40,000 kwa siku na kufikia Sh. 50,000 hadi 60,000 kwa siku.

Kwa upande wake Msimamizi wa Fedha za mkopo wa Benki ya Dunia chini ya fedha za uboreshaji miji (ULGSP) na Mhandisi wa TARURA Manispaa ya Morogoro, James Mnene, alisema mradi huo umegharimu Sh. milioni 644.

**Napongeza hatua ambazo manispaa imezichukua zinatufanya kuelekea kuwa Jiji, nafahamu ipo stendi kuu ya daladala Mafiga, soko kuu la kisasa, na miradi mingine ambayo inaendelea...**

**HABARI KIMATAIFA**

# Kamala Harris makamu rais wa kwanza mwanamke Marekani

**WASHINGTON,** MAREKANI



Rais mteule wa Marekani, Joe Biden na Makamu wa Rais, Kamala Harris, wakiwa wamenyanyua mikono yao juu ikiwa ni ishara ya ushindi baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa kufuatia uchaguzi mkuu wa nchi hiyo, Novemba 3, mwaka huu. Harris (picha ndogo), anakuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo katika taifa lenye nguvu kubwa kiuchumi duniani. **PICHA/BBC**

MAKAMU wa Rais mteule, Kamala Harris, ameweka historia na rekodi duniani kwa kuwa mwanamke wa kwanza, mwenye asili ya Kiafrika na Kiasia kushika nafasi kubwa ya pili ya nchini Marekani.

Harris, mwenye umri wa miaka 56, anaweza pia kuteuliwa kuwa mgombea wa kiti cha urais kupitia Chama cha Democrats, mwaka 2024.

Kwa mujibu wa uchambuzi wa masuala ya kisiasa nchini humo ni kwamba, huenda rais mteule, Joe Biden, ambaye hadi Januari, 2021 atakuwa amefikisha miaka 78, hataamua kugombea tena na kumalizia muhula wake wa pili.

Harris, alijitoa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania urais Desemba, mwaka jana, baada ya kutofanikiwa kushinda katika mchuano wa uteuzi wa kiti cha urais wa Chama cha Democratic.

Mwaka 2015 alianza kugombea nafasi ya seneta ya Marekani akachaguliwa 2016 na mwaka 2019 alitangaza kuanza kampeni ya kuwa mgombea wa Chama cha Democratic kwa nafasi ya urais wa Marekani kwenye uchaguzi wa miaka huu.

Licha ya Harris, kuacha kampeni hiyo, Agosti mwaka huu, aliteuliwa na Biden, kuwa mgombea mwenza kama makamu wa rais.

Harris kufikia hatua hiyo ya uongozi kama mwanamke, pia iliwahi kupigiwa chapuo mwaka 2017, na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Condoleezza Rice, alipotoa wito kwa wanawake kutokubali kubaguliwa sababu ya jinsia.

"Msikubali mtu yeyote kuwabagua kwa misingi ya kijinsia au rangi ya ngozi. Lazima tuwaambie wanawake: Unapoingia katika chumba cha mkutano, ikiwa mtu atajaribu kukudunisha, usikabiliane naye.

Unachotakiwa kufanya nikujieleza kwa utulivu bila hasira. Ikiwa unahisi huenda umezuiliwa kitu ambacho unadhani ulistahili kupata, kuna njia nyingi ya kukitafuta na una haki ya kuhakikisha unakipigania hadi ukipate." Rice alisema akiwa katika kongamano la uongozi la KPMG.

**HISTORIA**

Harris, amekuwa seneta California tangu mwaka 2016 hadi mwaka huu, alizaliwa Oktoba 20, mwaka 1964.

Alianza kuonekana utendaji wake baada ya kuwa mwanasheria wa kwanza mwanamke wa Wilaya ya San Francisco na pia mwanasheria mkuu wa kuteuliwa wa kwanza California.

Utawala wa Biden, ulimwona mwanamama huyu ambaye ni mtoto wa wahamiaji kutokea India na Jamaika, wakati akishughulikia masuala ya ubaguzi wa rangi.

Harris, baada ya Marekani kukumbwa na maandamano ya kupinga ubaguzi wa rangi hasa kwa watu walio na asili ya kiafrika dhidi ya polisi, alikuwa mshauri mkuu kuhusu masuala hayo kwenye mahakama.

Baba yake Harris aliitwa Prof. Donald J. Harris mwenye asili ya India, mtafiti wa kansa Shyamala Gopalan alizaliwa mwaka 1938.

Wazazi wa Harris walipotengana, alihama pamoja na mama yake kwenda nchini Canada hadi alipohitimu elimu ya sekondari.

**WASIFU**

Harris ambaye ni mwanasiasa na wakili, ameolewa na mwanasheria, Douglas Emhoff, wana watoto wawili.

Pia alikuwa Mwanasheria Mkuu wa 32 wa California kati ya mwaka 2011 hadi 2017 na Mwanasheria Mkuu wa 27 wa San Francisco tangu mwaka 2004 hadi 2011.

Alisoma siasa, uchumi na sheria nchini Marekani hadi kuhitimu uzamivu wa sheria mnamo 1989.

Alianza kazi kwenye ofisi za wanasheria wa serikali hadi kuchaguliwa kuwa mwanasheria mkuu wa jiji la San Francisco mwaka 2004 kama mgombea wa Democrat.

**...Joe Biden aapa kuwaunganisha Wamarekani**

Mteule, Joe Biden, amesema atayaponya makovu ya vidonda kwa Wamarekani baada ya kupata ushindi, akitoa hotuba yake ya kwanza rais mteule, huku akiapa kwamba hatoligawa taifa hilo, badala yake ataliunganisha.

"Tumpatie kila mtu fursa," alisema Biden.

Biden alimshinda rais aliyekuwa madarakani, Donald Trump, baada ya kura kuhesabu licha ya mchakato kukumbwa na hisia tofauti baada ya uchaguzi wa Novemba 3, nchini humo.

Trump, bado hajakubali kushindwa na hajazungumza hadharani, tangu yalipotangazwa matokeo.

Matokeo hayo yanamfanya Trump, kuwa rais wa kwanza aliyehudumu kwa muhula mmoja tangu miaka 90.

Kamati yake ya kampeni, iliwasilisha kiwango kikubwa cha kesi katika majimbo kadhaa, licha ya maofisa wa uchaguzi kusema hakuna ushahidi kwamba kulikuwa na udanganyifu katika uchaguzi huo dhidi yake.

Sherehe kadhaa zilizuka katika miji mikuu, baada ya vyombo vya habari kutangaza, Biden alishinda mwishoni mwa wiki.

Wafuasi wa Trump, walikuwa wamekasirishwa na matokeo hayo katika baadhi ya miji, hakukuwapo na ripoti za matukio yoyote.

Biden: "Lazima tuache kuwachukulia wapinzani wetu kama maadui zetu. Naahidi kuwa rais ambaye angependelea kuwaunganisha na sio kuwagawanya, ambaye hatazami majimbo mekundu na ya bluu bali Marekani kwa pamoja."

Biden, aliyeshinda kura milioni 74, ndiye rais aliyeweza kupata kura nyingi zaidi za wananchi.

Rais huyo mteule, ambaye aliwasilisha katika jukwaa akivalia barakoa, alitangaza kwamba atabuni kamati yake ya kukabiliana na virusi vya corona, ili kuhakikisha inaidhinisha maamuzi atakayotoa siku ya kuapishwa kwake Januari, mwakani.

Trump alikosolewa na Biden katika hatua zake kukabiliana na COVID-19.

Mapambano ya mlipuko wa virusi hivyo uliokuwa katikati ya kampeni za urais, yalikosolewa pakubwa na Biden, huku zaidi ya Wamarekani 237,000 wakifariki dunia, idadi iliyo kubwa kuliko taifa lingine duniani.

Harris akiwahutubia wafuasi wake: Wakati ambapo demokrasia yetu ilikuwa hatarini dunia nzima ilikuwa inatazama na mkawapatia Wamarekani siku mpya."

"Mlichagua matumaini, heshima sayansi na ukweli - mlimchagua Biden kuwa rais wa Marekani. Na barabara mbele haitakuwa rahisi, lakini Marekani iko tayari na hivyo basi mimi na Joe pia tuko tayari."

Harris alikuwa na jukumu kubwa katika ukusanyaji wa pesa za kampeni za Biden hususan katika miezi ya mwisho ya kampeni, na kusababisha msisimko mkubwa kwa kufanya wafadhili wa chama hicho kujitokeza zaidi.

Biden alishinda Jimbo la Pennsylvania lenye idadi ya wajumbe 20 na ushindi huo kumpatia mgombea huyo wa Democratic wajumbe 273. **BBC/REUTERS**

## Miili 17 yagundulika katika makaburi ya pamoja Libya

**Tarhuna,** LIBYA

MIILI ya watu 17 imegunduliwa katika makaburi ya pamoja, Magharibi mwa Libya, mkoani Tarhuna.

Kugundulika huko kunafanya jumla ya miili iliyofukuliwa katika miezi ya hivi karibuni kufikia 112.

Lotfi Tawfiq, ambaye anaongoza timu ya kuwatafuta watu ambao wamepotea, alisema miili hiyo, ilibainika Alhamisi wiki iliyopita, baada ya kufukuliwa makaburi matano tofauti.

Makaburi hayo yapo eneo la Tarhuna, mahala ambako mbabe wa kivita Khalifa Haftar, alianzisha mashambulizi yake kuelekea Tripoli. **DW**

# DESCHAMPS ATOA NENO KUMWACHA UPAMECANO



**PARIS,** Ufaransa

DIDIER Deschamps anaamini Dayot Upamecano, anapitia "wakati mgumu" baada ya mlinzi huyo kuachwa kwenye kikosi cha Ufaransa.

Deschamps amesema nyota huyo wa RB Leipzig, Upamecano mwenye umri wa miaka 22 ambaye ameichezea mechi tatu Ufaransa, anaweza kupata nafasi kwa siku za usoni.

"Kuna ushindani mkubwa katika nafasi hii. Alikuwa na sisi hapo kabla. Anapitia wakati mgumu kwa sasa," alisema kocha huyo wa Ufaransa akiwaambia waandishi wa habari.

"Anajua anaweza kufanya vizuri zaidi. Alikuwa mtulivu Septemba wakati tulipomuita kwa mara ya kwanza na Oktoba. Ni kijana mdogo na ana nafasi nzuri tu. Anacheza mechi nyingi.

"Bila shaka kama si yeye ni mwingine, ni kuhusu ushindani. Kurt Zouma ambaye anafanya vizuri kule Chelsea anaijua vizuri timu ya Taifa ya Ufaransa.

"Mlango haujafungwa. Nimefanya uchaguzi huo leo kwa sababu maalumu. Na inaweza kuwa hivyo hivyo kwa Machi na Juni?

"Ni jambo la kawaida kwa wachezaji wote ambao hawajaitwa, lakini wanaweza kuwa na matumaini ya kuitwa kwenye timu ya taifa."

# Maddison alia kutemwa England

**LONDON,** England

JAMES Maddison amekubali kwamba amekatishwa tamaa kwa kuondolewa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England, lakini ameahidi kupambana ili arejeshwe.

Gareth Southgate alithibitisha kikosi chake kitakachoivaa Ireland, Ubelgiji na Iceland, lakini hakumuita nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, wakati akitangaza kikosi hicho Alhamisi.

Maddison kwa sasa hajajumuishwa kwenye kikosi hicho tangu alipoitwa kwa mara ya kwanza kwenye mchezo dhidi ya Montenegro, Novemba mwaka jana.

Alipoulizwa kama alijisikia vibaya kwa kuondolewa kwenye kikosi hicho, Maddison nyota wa Klabu ya Leicester City aliiambia BT Sport: "Ndio, nimejisikia vibaya.

"Nataka kuwa kwenye kikosi cha England, hicho ndicho nilichokiota tangu utotoni. Napenda kuichezea timu yangu ya taifa.

"Niko fiti, lazima nipambane kuhakikisha naitwa tena kwenye kikosi hicho. Nilikuwa na majeruhi kwa muda mrefu.

"Kwa sasa nahitaji kupambana kwa nguvu zaidi ili niwezi kurudi kwenye timu hii, maana nataka kutimiza ndoto yangu ya muda mrefu."






# *Arteta amkomalia Pepe*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta bado anataka ubora mwendelezo kutoka kwa Nicolas Pepe baada ya mshambuliaji huyo kufunga wakati wakishinda 4-1 kwenye Ligi ya Europa dhidi ya Molde.

Pepe alifunga na kutoa pasi ya mwisho wakati Arsenal ilipojivuta kileleni mwa msimamo wa Kundi B.

Nyota huyo wa kimatafa wa Ivory Coast, ambaye alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 72 mwaka jana, ana mabao mawili na pasi za mwisho mbili kwenye Ligi ya Europa msimu huu, lakini ameanza katika mechi moja tu kwenye Ligi Kuu ya England.

Na sasa kocha wa Arsenal, Arteta anataka Pepe kuendelea kuwa kwenye kiwango bora zaidi wakati wakapocheza na Aston Villa kwenye Ligi Kuu, Jumapili.

"Kiwango mwendelezo katika kila mchezo, kwa dakika zote 90, kwenye kila mchezo, na naamini anaweza kufanya vizuri zaidi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunahitaji zaidi uwezo wake kwa sasa. Alifunga bao bora na kutoa pasi za mwisho na anaweza kufanya mengi zaidi uwanjani.

"Kiujumla anatakiwa kuwa kwenye kiwango chake katika mchezo, kila wiki na kwenye mechi zote."

HABARI MICHEZO

# United kumkosa Pochettino

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United ipo hatarini kuikosa huduma ya kocha Mauricio Pochettino kama hawataamua mapema kumtimua kocha aliye katika presha kwa sasa, Ole Gunnar Solskjaer, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Kuna uwezekano wa Man United kumchukua kocha wa zamani wa Tottenham, Pochettino kuziba nafasi ya Solskjaer, ambaye yupo katika hatari ya kutimuliwa.

Pochettino amekuwa bila timu kwa mwaka mmoja sasa tangu alipotimuliwa Spurs, lakini kuonekana katika kipindi cha Sky Sports cha Jumatatu ilikuwa dalili njema.

Inaaminika kuwa kocha huyo raia wa Argentina amefanya mazungumzo na mmoja wa viongozi wa juu wa klabu hiyo wiki chache zilizopita juu ya kurudi kazini.

Pochettino anatajwa kama mtu sahihi wa kumrithi Solskjaer, lakini Man United haitakuwa na wazo hilo kwa sasa.

Bado klabu hiyo inaendelea kumpa sapoti Solskjaer, hata hivyo inaweza kuikosa saini ya Pochettino kama watamtimua kocha wa sasa wa miamba hiyo ya Old Trafford.

Nafasi ya Solskjaer kwa mara nyingine imekuwa katika wakati mgumu baada ya wiki moja iliyopita kuchapwa na Arsenal, kabla ya kuchapwa na Istanbul Basaksehir kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na ikashinda juzi dhidi ya Everton.





# KANE AWEKA REKODI YA MABAO

**LONDON,** England

NYOTA wa Klabu ya Tottenham Hotspur, Harry Kane, ameweka rekodi ya kufikisha jumla ya mabao 200 klabuni hapo.

Kane alifikisha idadi hiyo baada ya kufunga bao moja katika ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Ludogorets kwenye Ligi ya Europa, Novemba 5, mwaka huu.

Anakuwa ni mchezaji wa tatu kufikisha idadi ya mabao hayo ndani ya Spurs akiwa nyuma ya Bobby Smith mwenye mabao 208 na Jimmy Greaves aliyefunga mabao 266.

Kane ametupia jumla ya mabao 12 kwenye michuano yote msimu huu na ametoa jumla ya pasi za mwisho 10 hadi sasa.

# Tuchel atoa sababu kumpa nafasi Kean

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Thomas Tuchel anaamini ni ngumu sana kutomchezesha Moise Kean baada ya mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain kuendelea kufunga.

Kean, ambaye anacheza kwa mkopo pale PSG kutoka Everton, alifunga bao lake la tano wakati timu hiyo ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Rennes kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, ana mabao matatu katika mechi nne za Ligue 1 zaidi ya mawili ambayo alifunga Ligi Kuu England akiichezea Everton katika mechi 31.

Tuchel alisifia kiwango cha Kean pale PSG, ambao wanaongoza kwa pointi tano kileleni mwa msimamo.

"(Kean) ana moyo wa kupambana, ana uwezo wa kucheza vizuri. Haogopi na ni mtu ambaye anapenda kuona akicheza kila mechi.

"Ni ngumu sana kusema unamuacha benchi, hivyo lazima apate nafasi ya kucheza kila wakati.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CAVANI AWEKA REKODI EPL KAMA IBRAHIMOVIC

**Awa 'mzee' wa pili kufunga bao katika ligi hiyo wakati wakiibanjua Everton kwa...**

**LIVERPOOL,** England

WAKATI Edinson Cavani akiweka rekodi yake Ligi Kuu England, Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema walikuwa na muda mchache wa maandalizi, baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Everton, juzi Jumamosi.

Katika mchezo huo uliyopigwa Uwanja wa Goodison Park, Cavani akiwa na umri wa miaka 33 na siku 267, amekuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga bao kwenye mechi yake ya kwanza Ligi Kuu England tangu Zlatan Ibrahimovic alipofanya hivyo Agosti 2016 wakati huo akiwa na umri wa miaka 34 na siku 316.

**Man United walitoka kuchapwa kwenye Ligi ya Mabingwa kule Uturuki na kuingia moja kwa moja kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England.**

"Tuliwasili Alhamisi, hivyo tulikuwa na siku moja tu ya kujiandaa. Lakini nawapongeza wachezaji wangu wameonyesha hali ya kupambana na kusababisha tupate ushindi huu muhimu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

Solskjaer alionekana kushusha pumzi baada ya kipindi kigumu cha kupoteza mechi mbili mfululizo.

Everton ndio ilikuwa ya kwanza kupata bao la kuongoza katika dakika ya 19 kutoka kwa Bernard, kabla ya Man United kusawazisha kupitia Bruno Fernandes dakika ya 25.

Cavani aliyesajiliwa kutoka PSG kwa uhamisho huru alishindilia msumari wa moto katika dakika za nyongeza na kufanya ubao usome 3-1.

Huo unakuwa ni mchezo wa tatu mfululizo kwa Everton ambayo ilikuwa nyumani kucheza bila ya kupata ushindi, ambapo michezo mitatu iliyopita ilikubali kufungwa miwili na kutoka sare mmoja.

Baada ya matokeo hayo, Man United imepanda hadi nafasi ya 14, ikiwa imefikisha alama 10 baada ya kucheza mechi saba.

Wao Everton wakisalia nafasi ya tano kwa alama zao 13 baada ya kucheza mechi nane.

## ZISIKUPITE

### BECKHAM AMTAKA RAMOS

DAVID Beckham anataka nahodha wa Real Madrid, Sergio Ramos kuichezea Inter Miami wakati mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 utakapomalizika msimu ujao. ***(AS)***

### FODEN KUULA MAN CITY

KIUNGO wa Manchester City na England, Phil Foden mwenye umri wa miaka 20, anatarajiwa kupatiwa mkataba mpya ambao utaongeza mara tatu mshahara anaopata kwa sasa. ***(Star on Sunday)***

### WEST HAM KWA DEMBELE

KLABU ya West Ham United inatarajiwa kuwasilisha ombi la pauni milioni 30 ili kumnunua mshambuliaji wa Lyon na Ufaransa, Moussa Dembele, 24, iwapo klabu hiyo itaamua kumuuza mchezaji huyo. ***(Sun on Sunday)***

### ARSENAL IMEMSHINDWA AOUAR

KOCHA wa Klabu ya Lyon, Vincent Ponsot, amefichua kwamba Arsenal ni miongoni mwa klabu tatu ambazo zilikuwa zinamnyatia kiungo wa kati wa Ufaransa, Houssem Aouar, 22, katika dirisha la uhamisho lililopita, lakini ilitoa dau la chini ya kuliko thamani ya mchezaji huyo. ***(Sport Witness)***

### DIABY ALIKATALIWA

TIMU ya Bayer Leverkusen ilikataa kuanzisha mazungumzo na Manchester United kuhusu uwezekano wa kumuuza winga wa Ufaransa, Moussa Diaby katika dirisha la uhamisho lililopita. ***(Bild)***

### PODOLSKI AMTETEA OZIL

ALIYEKUWA mshambuliaji wa Arsenal, Lucas Podolski ambaye kwa sasa anaichezea klabu ya Uturuki ya Antalyaspor amemkosoa kocha Mikel Arteta kwa jinsi wanavyomfanyia Mesut Ozil. ***(Bild, via Goal)***

### ROMERO AJIFUA MAN UTD

GOLIKIPA wa Argentina, Sergio Romero, 33, anafanya mazoezi akiwa peke yake katika klabu ya Manchester United, akitumaini kuachiwa kuondoka katika klabu hiyo kwa uhamisho wa bila malipo Januari. ***(Sun on Sunday)***

### KANE MATUMAINI KIBAO

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, anaamini Spurs ina fursa nzuri ya kushinda Ligi Kuu ya England msimu huu. ***(Sunday Mirror)***

### GERRARD AWEKA MSIMAMO

KOCHA wa Klabu ya Rangers, Steven Gerrard, anasisitiza kuwa sasa si wakati wa kuzungumzia mkataba mpya wa kiungo Steven Davis mwenye umri wa miaka 35 anayeichezea Ireland. ***(Scottish Herald)***

### ARTETA HAJUTII KWA MARTINEZ

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta hajutii kumuuza kipa wa Argentina, Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 28, katika klabu ya Aston Villa. ***(Sunday Mirror)***

### YAJITOA KWA SIMAKAN

KLABU ya Marseille imejiondoa katika ushindani wa kumsajili mchezaji wa Strasbourg, Mohamed Simakan, mwenye thamani ya pauni milioni 20. ***(Birmingham Mail)***

## Azam FC, Yanga kuamua Nov. 25

**Na Mwandishi Wetu**

LIGI Kuu Bara imekwenda mapumziko kupisha Kalenda ya Fifa, huku Azam FC ikiendelea kutawala kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo baada ya kujikusanyia pointi 25 moja mbele ya Yanga baada ya timu zote 18 zinazoshiriki ligi hiyo kushuka dimba mara 10 hadi sasa.

Hata hivyo, mbio za ubingwa wa ligi hiyo msimu huu zinaonekana kuwa za farasi watatu, Azam, Simba na Yanga ambazo kila moja imepania kutwaa taji hilo ambalo 'Wekundu wa Msimba' wenyewe wakitaka kulibeba kwa mara ya nne mfululizo.

Katika mbio hizo, Yanga inayoshika nafasi ya pili ikiwa na pointi 24, nne mbele ya Simba, itakuwa na mechi ya kuamua timu itakayokaa kileleni dhidi yake na Azam Novemba 25, mwaka huu, lakini nafasi hiyo ikitegemea zaidi kupata kwanza matokeo mazuri ya mechi zao dhidi ya Namungo na KMC.

Ligi hiyo inatarajiwa kurejea tena Novemba 20, mwaka huu kwa timu mbalimbali kushuka dimbani, lakini siku moja baadaye Simba itakuwa ugenini dhidi ya Coastal Union wakati KMC FC ikiikaribisha Azam FC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Novemba 22, Yanga itashuka uwanjani kuikaribisha Namungo ikiwa inajua matokeo ya Azam dhidi ya KMC, endapo ikishinda itakaa kileleni kama 'Wanalambalamba' hao watapoteza ama kutoka sare, vinginevyo itazidi kumfukuza 'mwizi' kimyakimya.

Baada ya mechi hizo, Novemba 24, Simba itaelekea ugenini katika Uwanja wa Samora kuivaa Dodoma Jiji wakati kesho yake kukiwa na vita kali kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, wakati wenyeji Azam FC watakapoikaribisha Yanga.

Kama Azam na Yanga kila moja itashinda mechi yake zitakapocheza dhidi ya KMC na Namungo, mchezo huo utakaozikutanisha ndio utaamua timu itakayokaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

# FEI TOTO ALIA NA RIZIKI KUKOSA 3 ZA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', amesema kukosa ushindi kwenye mechi dhidi ya Simba ilikuwa si riziki yao tu, na kwamba wamebakiza dakika tano tu ili wazoe pointi zote tatu.

**Akizungumza baada ya mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, Fei Toto alisema walijitahidi kwa kila hali ili kuhakikisha wanashinda, lakini mambo yalikwenda ndivyo sivyo.**

"Huu ulikuwa ni mchezo mkubwa, ukimuwahi mwenzako ni lazima ufanye mipango ili umdhibiti. Ndiyo maana unaona tulivyopata bao tulifanya kazi ya kujilinda na kushambulia kwa kushtukiza na hii ilikuwa ni mipango ya mwalimu, kifupi tulikuwa bora sana, lakini haikuwa riziki yetu," alisema kiungo huyo ambaye anaichezea timu ya Taifa ya Zanzibar, Zanzibar Heroes.

Kwa upande wa Kibwana Shomari, alisema sare waliyoipata si mbaya na watajipanga kwa mechi nyingine.

"Mpira ni mchezo wa kuwahiana, namshukuru Mwenyezi Mungu nimecheza vizuri na pia wachezaji wenzangu wamecheza vizuri, lakini tulipata bao, na wao baadaye wakarudisha, tulikuwa tutoke na pointi tatu, lakini tumepata moja, hivyo tunajipanga kwa mechi zinazokuja," alisema mchezaji huyo ambaye ni 'dabi' yake ya kwanza, akisajiliwa msimu huu kutokea Mtibwa Sugar.

Naye beki wa Simba, Joash Onyango alisema 'dabi' ilikuwa ngumu kwa sababu Yanga walicheza vizuri, lakini wamejitahidi hadi wamepata bao la kusawazisha.

Kuhusu kuitwa babu na wapinzani wake, alisema kuwa hana shida na hilo, ila amewaonyesha jinsi gani babu anaweza kufanya.

"Vyovyote watakavyoniita mimi sijali, hata watafute jina lingine mimi sina tatizo, ila nimewaonyesha jinsi gani babu anavyoweza kufanya mbele ya vijana," alisema Onyango aliyesajiliwa msimu huu akitokea Gor Mahia ya Kenya.




Mabondia wa Tanzania, Hassan Mwakinyo (kulia) na Zulfa Macho wanaotarajia kupanda ulingoni Ijumaa wiki hii katika Ukumbi wa Next Door Arena, Oysterbay jijini Dar es Salaam, kuvaana na Muargentina Jose Carlos Paz na Mzimbabwe Alice Mbewe. **MPIGAPICHA WETU**

# *Rais WBF kusimamia pambano Mwakinyo, Muargentina*

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Chama cha Ngumi za Kulipwa cha WBF, Howard Goldberg atawasili nchini Jumatano kwa ajili ya usimamizi wa pambano la ubingwa wa mabara super-welterweight kati ya bondia Hassan Mwakinyo na Jose Carlos Paz wa Argentina lililopangwa kufanyika kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Oysterbay Ijumaa wiki hii.

Goldberg atawasili pamoja na mwamuzi wa pambano hilo, Edward John Marshall saa 3:15 asubuhi kwa ndege ya Shirika la Ndege la Kenya, KQ.

Mbali ya kuwa Rais wa WBF, Goldberg enzi zake alikuwa mwamuzi na jaji wa ngumi za kulipwa duniani akiwa amecheza zaidi ya mapambano 300 katika nchi mbalimbali.

Goldberg anakuja nchini kwa mara ya sita kwa ajili ya kusimamia ngumi za kulipwa na amefurahishwa sana na weledi wa Kampuni ya Jackson Group Sports katika pambano hili kwani kutokana na kukamilisha masharti yote ikiwa ni pamoja na tiketi za ndege za ujio wao.

Alisema Kampuni ya Jackson Group Sports imeonyesha njia chanya katika kuandaa mapambano ya ngumi za kulipwa kwa weledi na uwazi mkubwa, jambo ambalo limewafanya wao kutoa kibali na kuja kusimamia pambano la Mwakinyo dhidi ya Paz.

Alisema kuwa kila kitu ambacho WBF ilikihitaji kutoka kwa waandaaji wa pambano hilo, kilipatikana na kukamilishwa haraka, jambo ambalo limewapa faraja kubwa. Kwa mujibu wa Goldberg, ujio wa Jackson Group Sports kwenye ngumi, ni fursa kwa mabondia wenye lengo la kupata maendeleo na anaamini Tanzania (kupitia Jackson Group Sports) itapata mabondia wengi wenye vipaji.

Alisema ametembelea nchi zaidi ya 60 duniani kwa kazi ya kusimamia mapambano ya WBF, lakini amekuwa na furaha zaidi kuja Tanzania yenye vivutio vikubwa vya utalii ikiwa ni pamoja na hifadhi ya Serengeti na Zanzibar.

"Nimekuwa nikiulizwa na baadhi ya maofisa wa WBF kwa nini napenda kuja Tanzania, jibu ni rahisi sana, ni nchi yenye uzuri wa asili na vivutio vingi vya utalii, wananchi wake wana upendo mkubwa na ushirikiano ambao nimekuwa nikiupata na serikali kupitia Wizara ya Michezo na mapromota," alisema Golberg.

Wakati huo huo; bondia Fatuma Zarika atawasili nchini leo kwa ajili ya pambano lake dhidi ya Patience Mastara wa Zimbabwe ambaye naye anatarajiwa kuwasili kesho usiku.

Mkurugenzi wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema Zarika atawasili saa 3.30 usiku tayari kwa pambano hilo na kwamba mpinzani wa Mwakinyo, Paz ameshawasili nchini na anaendelea kujifua.

Alisema mabondia wengine, Alex Kabangu kutoka DR Congo ambaye atazichapa na Hussein Itaba wa Tanzania, atawasili kesho usiku, huku mpinzani wa bondia Zulfa Macho wa Tanzania, Alice Mbewe akiwasili nchini leo.

Twissa alisema kila kitu kiko katika hatua za mwisho na tiketi zitaanza kuuzwa kwa njia ya Nilipe na Selcom kwa Sh. milioni tatu kwa meza ya watu 10 na Sh. 150,000 kwa viti vya kawaida.

# Michezo

Jumatatu Novemba 9, 2020

Nipashe





Wakali 10 wa mabao Ligi ya Mabingwa Ulaya UKURASA 12


**LA UZEENI...**



Mshambuliaji wa Manchester United, Edinson Cavani, akikamilisha ushindi wa mabao 3-1 wakati wakiichapa Everton kwenye Uwanja wa Goodison Park juzi. Kwa bao hilo Cavani anakuwa mchezaji 'mzee' zaidi baada ya Zlatan Ibrahimovic kuziona nyavu mechi yake ya kwanza Ligi Kuu England. **HABARI UK. 22**

# SVEN ALIA NA MAREFA, CEDRIC KIKOSI KIPANA

## ●●● Aitaja pia penalti katikati sare ya Simba, Yanga, kila mmoja afunguka kivyake, lakini...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, akilia na waamuzi kwamba ndio wameipa sare Yanga kwa kuwaondoa mchezoni wachezaji wake baada ya kushindwa kuwalinda kutokana na faulo mbaya walizokuwa wakifanyiwa, mwenzake Mrundi Cedric Kaze wa Wanajangwani hao, amesema kukosa kikosi kipana kama wapinzani wao kumewanyima ushindi.

**Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, shukrani kwa straika Mghana, Michael Sarpong aliyeifungia Yanga dakika ya 16 kwa penalti kabla ya beki Mkenya Joash Onyango kuisawazishia timu yake dakika ya 86, akiunganisha nyavuni kwa kichwa mpira wa kona uliopigwa na Luis Miquissone.**

Lakini Sven anaamini amekosa ushindi kutokana na maamuzi mabovu huku Kaze yeye akiamini kuumia kwa beki na nahodha wao, Lamine Moro pamoja na kutokuwa na kikosi kipana ndicho kilichowakosesha ushindi.

Makocha hao walitoa kauli hizo baada ya kumalizika kwa dakika 90 za mtanange huo, ambao mashabiki wengi walijazana nje ya uwanja kutokana na kukosa tiketi kwa sababu za changamoto za mtandao.

Sven alisema mchezo wao ulikuwa mzuri na ushindani mkubwa na wachezaji wake walicheza kiufundi na kimbinu zaidi katika dakika zote 90, lakini waamuzi walishindwa kumudu mchezo huo baada ya kutotoa maamuzi wanapocheza faulo.

Alisema licha ya faulo ambazo walifanyiwa wachezaji wake, lakini walinyimwa penalti ya wazi hali ambayo ilizidi kuwatoa mchezoni na kuishia kupata pointi moja.

"Mchezo ulikuwa na ushindani mkubwa sana, lakini waamuzi wameharibu mechi kwa sababu ukiangalia kwa umakini, wachezaji wangu walichezewa faulo na kunyimwa penalti, kuhusu ufundi, akili na mbinu tulikuwa juu zaidi, kwa hilo wachezaji wangu niwapongeze kwa kujitahidi hasa kutokana maamuzi ya waamuzi waliochezesha," alisema kocha huyo.

Alisema ilikuwa vigumu kuamini kwamba ameambulia sare kutokana na maandalizi waliyoyafanya, na kama waamuzi wangechezesha mchezo huo kwa umakini bila ya kuangalia upande mmoja, ana imani wangeibuka na ushindi katika mchezo huo.

"Niwasifu Yanga wamecheza vizuri kipindi cha kwanza kwa kuzuia njia zetu, ila kipindi cha pili vijana wangu wamefanya vizuri zaidi na kutumia mapungufu yao kupata bao la kusawazisha, lakini tumekosa nafasi ya wazi aliyopiga John Bocco kwa kichwa," alisema kocha huyo.

Kwa upande wa Kaze, alisema wachezaji wake walionyesha bidii kwenye kusaka matokeo kipindi cha kwanza ila mambo yalibadilika kipindi cha pili na kuwa magumu kwao baada ya kuumia na kufanyiwa mabadiliko kwa Lamine, hivyo kuliwafanya wachezaji wake kushindwa kujiamini.

"Pia ukosefu wa wachezaji bora kwenye benchi letu, unapomtoa mchezaji anayeingia anatakiwa kwenda kubadilisha mchezo na kutorudia makosa ya aliyotoka, ila kwangu ni toafuti kabisa kwa sababu wale ambao waliingia kuchukua nafasi ya walishindwa kunipatia kile nilichokuwa nakitaka.

"Ni tofauti na wenzetu ambao anayetoka na kuingia hawajapishana na walifanikiwa kubadilisha mchezo hasa kipindi cha pili, Simba wamecheza mpira mzuri na kuvutia na kutumia makosa yetu kupata bao la kusawazisha," alisema Kaze ambaye hiyo ni mechi yake ya nne kuiongoza Yanga.

Kaze alisema wachezaji wake walicheza vizuri kipindi cha kwanza ila cha pili mambo yalikuwa magumu kwa upande wao jambo ambalo liliwafanya waruhusu bao, walikuwa wanacheza na timu ambayo ina muunganiko wa muda mrefu.

# Onyango: Babu hawezi kuwafunga

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akiibuka shujaa wa Simba baada ya kuokoa jahazi dakika nne kabla ya kuzama Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, beki kisiki wa timu hiyo, Mkenya Joash Onyango, amewajibu mashabiki wa Yanga wanaomuita babu akisema "babu hawezi kuwafunga".

Katika mechi hiyo ya 'Dabi' ya Dar es Salaam iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1, Yanga ilikuwa ya kwanza kupata bao la kuongoza lililozamishwa kimyani kwa mkwaju wa penalti dakika ya 31 na straika Mghana Michael Sarpong.

Penalti hiyo ambayo katika marudio ya video inaonyesha ilistahili kuwa faulo ndogo kutokana Onyango kumwangusha, Tuisila Kisinda nje ya mstari wa 18, mwamuzi wa kati Abdallah Mwinyimkuu pamoja na wasaidizi wake watano, Ramadhani Kayoko, Aboubakar Mturo, Frank Komba, Mohamed Mkono na Elly Sassi, wamebebeshwa lawama kubwa kwa kushindwa kuumudu mchezo huo.

Lakini baada ya mechi hiyo, Onyango ambaye amekuwa akiitwa 'babu' na mashabiki wa upande wa pili, Yanga, wakieleza mwonekano wake hauendani na umri wake wa miaka 27, alipoulizwa anajisikia vipi kuitwa babu na kiwango alichokionyesha, alisema hana tatizo kwa vyovyote wanavyojisikia kumwita.

"Vyovyote watakavyoniita mimi sijali, hata watafute jina lingine mimi sina tatizo, ila nimewaonyesha jinsi gani babu anavyoweza kufanya mbele ya vijana.

"Mimi sina tatizo kuitwa jina lolote, hata wewe [mwandishi] wanaweza kukuita dada, vyovyote watakavyo, ila babu hawezi kuwafunga," alisema Onyango aliyesajiliwa msimu huu baada ya kumaliza mkataba wake na Gor Mahia ya kwao, Kenya.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >